

ISHARA YA WAKATI HUU



Mambo yote yawezekana, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu.

² Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa muda mfupi wa maombi. Baba yetu wa Mbinguni Mwenye neema, kwa kweli tuna furaha usiku wa leo, kwa ajili ya majaliwa ya kuja hapa New York, kuwahudumia watu Wako, katika Jina Lako. Tuna furaha sana kukutana nao, tukijua kwamba iko Kesho iliyo kuu ambapo tutakutana, ambapo kamwe hatutakuwa na maombi kwa ajili ya wagonjwa, kwa kuwa wagonjwa watakuwa na afya milele. Hakutakuwepo tena siku ndefu usiku wa maombi kwa ajili ya waliopotea, kwa sababu wote wataokoka wakati huo.

³ Na sisi tunatazamia siku hiyo ambapo Yesu atatokea. Tukiona saa inakaribia, na ishara na maajabu yanaelekeza kwenye wakati huo, inatufanya kusimama kwa muda mfupi, Bwana, kuwaza kuhusu nafsi zetu; sasa tunauliza swali hilo sasa, “Nichunguze na unijaribu, Bwana.” Na iwapo kuna uovu wowote ndani yetu, uondolee mbali, Baba. Sisi, sisi tunataka kukutumikia Wewe kwa moyo safi, mikono safi, kwa kuwa hatujui ni wakati gani Wewe utatuita na kutualika huko Juu. Tutakuja kukutana na Wewe.

⁴ Iwapo kuna wengine hapa ndani usiku wa leo, Bwana, ambao hawakujui Wewe kama Mwokozi wao, msamaha wa dhambi zao, wala hawajazaliwa kwa Roho wa Mungu, naomba huu uwe ndio usiku ambao watafanya uamuzi huo, na Mungu awajaze na wema Wake. Mponye kila mtu aliye mgonjwa, Baba, hapa ndani, wote wanaoteseka. Naomba kusiwe na mtu mnyonge katika jengo hili, wakati ibada hii ikimalizika, ama kusiwe na mwenye dhambi. Jalia tuone hili likitendeka kwa heshima na utukufu wa Mungu. Tunaomba hayo katika Jina la Mtoto Wake mpendwa, Yesu Kristo. Amina.

⁵ Ketini. Ni majaliwa makubwa tena kuwa hapa, usiku wa leo, kuhudumu tena katika Jina la Mwokozi wetu mpendwa, na Yule anayejitosheleza kwa yote.

⁶ Kama tulivyokuwa tukizungumza jana usiku juu ya Malaika wa Bwana, kwenye ishara kule Sodoma, kwamba wakati Malaika huyu alipobaki nyuma, kuzungumza na—na Ibrahimu; Mtu huyu ambaye alikuwa ni Malaika, lakini ilikuwa ni Mungu katika umbo la binadamu, kwa sababu Ibrahimu alimwita Yeye, “Bwana.” Msomaji yeyote wa Biblia anajua kwamba herufi kubwa B-w-a-n-a hutokana na “hapo mwanzo *Mungu* aliumba mbingu na nchi,” ambalo linamaanisha *Elohimu*, linamaanisha “Yule anayejitosheleza kwa yote, Yule Mwenyezi.” Na Mungu

alijitambulisha Mwenyewe hapo kwa Ibrahimu, katika umbo la mwanadamu. Msafiri tu aliyejaa vumbi, Hao walionekana kuwa hivyo. Kamwe hakusema mahali alikotoka. Bali tazama wakati Yeye angenena na Ibrahimu, Yeye alisema, “Nitafanya hili. Nilikuahidi hili.” Unaona? Na akamwita kwa jina lake—lake la “baba”, Ibrahimu, ambalo lilikuwa tu limebadilishwa kutoka kuwa Abram siku chache hapo kabla, bali sasa yeye ni Ibrahimu. Na kuitwa kutoka Sarai kuwa *Sarah*, “binti mfalme.” Ndipo basi Mungu akatoweka mbele za Ibrahimu, na kuenda huko chini Sodoma, na hiyo ilikuwa ndiyo ishara yao ya mwisho. Moto ulishuka kutoka mbinguni na kuangamiza Sodoma yote na Gomora, na miji iliyozunguka kote.

⁷ Ikionyesha, katika mfano, kile ulimwengu wa Mataifa utafanya. Utaangamizwa, utaangamizwa kwa moto. Mungu aliahidi hilo, kwamba Yeye hataangamiza ulimwengu tena kwa maji, kwa kutupatia ishara. Mungu kamwe hafanyi jambo bila ishara. Na Yeye alitupatia ishara ya upinde wa mvua, kama agano, Yeye kamwe hataangamiza ulimwengu tena kwa maji. Na, sasa, bali wakati huu ni moto.

⁸ Na kama vile Yesu alivyorejea nyakati, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, wakati safina ilipokuwa inaandaliwa, ambapo watu wanane pekee waliokolewa kwa maji, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu.” Waangalie wachache pale, “Kama ilivyokuwa, ambapo watu wanane waliokolewa kwa maji.” Ndipo Yeye akaendelea na kutoa maadili ya siku hiyo, “kula, kunywa, kuoa, kuolewa.” Na iwapo. . .

⁹ Nilikuwa nikisoma hilo wakati fulani uliopita na nilikuwa nikitoa maelezo juu yake, nikihubiri juu yake. Na ndipo nikashika, Yesu alisoma Mwanzo ule ule ambao ninasoma na wewe unasoma. Kwa hiyo nikarudi nyuma katika Mwanzo 6, kuona kile walichofanya katika siku hiyo, na tunaona ya kwamba “wana wa Mungu walijitwalia wenyewe binti za wanadamu.” Niliangalia tafsiri yao pale, kasema, “walijichukulia wanawake,” si mabinti. Hiyo ilikuwa tu kama Reno, Nevada; ndoa tu, talaka, kama Hollywood, na kadhalika. Na ndipo kasema, “hawa walikuwa ni watu mashuhuri, wa kale.”

¹⁰ Ndipo mliona jarida la *Life*, ambapo kashfa hii kubwa iliinuka huko Uingereza, ya wale watu mashuhuri, na wale makahaba na kadhalika, na jinsi ambavyo magavana wetu. Na, loo, jamani, ni lundo la jinsi gani tulilo ndani yake, hasa kabisa ile picha ambayo Yesu alisema ingetokea, unaona. “Wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa, nao hawakujua hilo mpaka siku ile Nuhu alipoingia ndani ya safina.”

¹¹ Na ndipo mlango ukafungwa. Hakukuwa na nafasi tena. Hayo yalikuwa ndiyo mahubiri yake ya mwisho. Mahubiri

ya mwisho ambayo yamehubiriwa katika huduma yoyote mashuhuri yamekuwa ni kwa wale wasioweza kuokolewa. Nuhu, ujumbe wake wa mwisho ulikuwa ni kwa wale wasioweza kuokolewa. Unaona, aliingia ndani nao mlango ukafungika nyuma yake, ndipo akakaa humo siku saba kabla ya kuanza kunyesha. Unaona, ujumbe wake kwanza ulikuwa kuhubiri, kujenga safina, na halafu akafungiwa siku saba.

¹² Watu wakasema, “Yule mzee mlokole. Unaona, yumo tu mle ndani, alifunga mlango mwenyewe.” Bali Mungu aliufunga. Kitu kile kile kilikuwa Sodoma.

¹³ Mtazame Bwana wetu Yesu. Wakati Yeye alipokuja duniani, Yeye alikuwa kijana Nabii wa Galilaya. Alienda katika masinagogi, kila mtu alimpenda. Aliwaponya wagonjwa. Hiyo ilikuwa ndiyo sehemu Yake ya kwanza ya huduma Yake, hatua ya kwanza. Hatua ya pili ilikuwa ni unabii, ambapo Yeye alianza kuwakemea Mafarisayo na Masadukayo wa siku Zake, kuwaambia kile walichokuwa na jinsi walivyokuwa vipofu na wasingeweza kuona Hilo, na kuwa Yeye alikuwa ni nani, na kadhalika, mwajua, na kile kilichokuwa kinaenda kuwafanyikia. Juu ya hili Yeye alihukumiwa, na juu ya misingi hii Yeye alisulubiwa, bali hawangeweza kukomesha Ujumbe. Unaweza kumkomesha mjumbe, bali si Ujumbe. Pia Biblia ilisema kwamba “Yeye alipaa akaingia kuzimu na kuzihubiria nafsi ambazo zilikuwa kifungoni, ambazo kwa wakati fulani hazikutii,” na hapo Ujumbe Wake wa mwisho ulikuwa kwa waliohukumiwa.

¹⁴ Litakuwa jambo la kutisha kuwazia, sasa, kwamba baadhi ya siku hizi kwamba watu watakuwa wanaendelea kuhubiri kama tu walivyofanya katika siku za Nuhu, wangukuwa wanaendelea tu vivyo hivyo, bali kwa ulimwengu uliohukumiwa ambao tayari milango imefungwa. Hatujui ni wakati gani hilo huenda likafanyika. Kwa hiyo ikiwa wewe si Mkristo, usiku wa leo, wazia hilo kwa nguvu kabisa. Liwazie kwa uzito.

¹⁵ Sasa kuna jambo moja tu ambalo tunajua kufanya, ni kufuata maagizo ambayo Bwana wetu alituachia, “Thubirini Injili kwa kila kiumbe.” Yeye anajua ni nani aliyeokoka na ni nani asiyeokoka. Sisi hatujui hilo. Tunatupa tu wavu baharini, kuleta wa kila aina, bali Mungu anajua ni nani ameokoka na ni nani hajaokoka. “Na hakuna mtu awezaye kuja Kwake isipokuwa Baba amemvuta; na wote ambao Baba amempa Yeye watakuja.” Tunajua hilo, unaona. Kwa hiyo sisi hatuwezi kusema *huyu* ni Mkristo na *yule* siye, kwa sababu Yeye alisema, “Ufalme wa Mbingu ni kama mtu aliyechukua wavu na kuenda baharini na kuutupa ndani. Wakati alipokuwa ameweka wavu huo ndani, alikuwa na kila namna za vitu hapo ndani. Kungekuwa na buibui wa majini, wadudu, nyoka, na samaki, na samaki mla mizoga, na samaki wazuri.” Na, lakini, unaona, wa—wadudu wa majini na kadhalika hatimaye wanatambaa na kurudi majini tena, bali

samaki wazuri waliwekwa kwa ajili ya Bwana. Sasa sisi hatujui ni yupi. Tunatupa tu wavu.

¹⁶ Lakini kumbuka, huyo mdudu wa majini alikuwa mdudu wa majini wakati wavu ulipoenda juu yake. Ushawishi wa mkutano ulikuwa ndio uliomshika. Nyoka alikuwa angali ni nyoka, wavu wa Injili ulimvuta tu ndani. Na samaki mla mizoga alikuwa samaki mla mizoga, kasa alikuwa ni kasa, kamba wa maji baridi alikuwa kamba wa maji baridi, unaona. Lakini samaki halisi alikuwa samaki, kwa kuanzia. Kwa hiyo Yeye anajua ni yupi, kwa sababu Yeye anayo majina yao kwenye Kitabu Chake, yaliwekwa pale wakati Mwana-kondoo alichinjwa kabla ya msingi wa ulimwengu.

¹⁷ Tupo hapa kujaribu kufanya sehemu yetu. Sasa Ndugu Vick amekuwa kule kwenye kona, akitupa wavu, kwa miaka mingi. Wahudumu wengine wamekuwa kwenye kona zingine, wakitupa wavu. Nimekuja kuunganisha wavu wangu pamoja nanyi ndugu, kusudi tuweze kutupa pakubwa, na tuendeleo tu kuvuta, kama wavuvi kwenye kona za ziwa. Mojawapo ya siku hizi, samaki wa mwisho atachukuliwa kutoka ziwani. Uvuvi utakuwa umeisha wakati huo. Hebu tumtafute Mungu kwa mioyo yetu yote, tuombe na tuwe wanyofu tunapoona saa hii ikikaribia.

¹⁸ Sasa, usiku wa leo tunaenda kuwaombea wagonjwa. Tunaitoa. Ninaamini Billy...sikapata kuzungumza...Je! alisambaza kadi za maombi? Wale...Naam. Vema, nenda... Sawa. Hilo ni jema. Vema.

¹⁹ Sisi, jana usiku, tulikuwa tunaenda kujenga kwa ajili ya usiku wa leo, kwa ajili ya ibada ya maombi. Ndipo basi nikafikiria labda nichukue siku moja au mbili usiku, kwa ajili tu ya kuhubiri. Basi tutaona ni wangapi hawajapokea Roho Mtakatifu. Na hilo ndilo jambo kuu, unaona. Kama uki—kama ukipata...Kama umeponywa, Mungu atakuponya, hakika. Yeye amefanya hivyo tayari. Inakubidi tu kuamini. Lakini kama umeponywa, utakuwa mgonjwa tena ukiishi muda mrefu kutosha, labda. Lakini wakati umeokoka, hiyo ni tofauti, unaona, hilo. Unaona?

²⁰ Na sasa tunaenda kusema jambo hili moja kwa sababu wakati mwingine kuna wageni wanaingia, ambao huenda wako mkutanoni, labda hawajawahi kuona ibada ya uponyaji. Na mara nyingi wanajaribu kubandika neno hilo juu yako, “mponyaji wa Kiungu.” Lakini hakuna...Kuna mponyaji mmoja tu wa Kiungu, huyo ni Mungu. Na, kwa kweli, kuna Mponyaji mmoja tu, huyo ni Mungu.

²¹ Sasa, madaktari hawadai kuwa waponyaji. Wao si waponyaji, hawadai kuwa. Vipi kama nilienda nje na kuvunja mkono wangu hapa nje, na kuingia ndani na kusema, “Daktari, ponya mkono wangu, upesi sana, i—inanibidi kumaliza kazi yangu”? Angesema, “Unahitaji uponyaji wa akili.” Vema,

hiyo, hiyo ingekuwa kweli. Unaona? Sasa daktari anaweza kuunganisha mkono wangu, bali Mungu hufanya uponyaji. Kama nikikata mkono wangu, niseme, “Daktari, nilikata mkono wangu, uponye upesi sana kwa ajili yangu.” Hawezi kufanya hilo. Jambo pekee analoweza kufanya ni kuuosha; kama umepanuka, anaweza kuushona; lakini inabidi Mungu auponye.

²² Unaona, maumbile hayana budi kujenga seli, uhai. Uhai lazima uweke huo pamoja. Mwili huo hauna budi kutoa kalishi, na kadhalika, na wenyewe una uhai. Kalishi haitaponya. Ni uhai. Unaona, hakuna dawa ambayo huponya. Dawa husafisha tu huku Mungu anaponya. Unaona? Hakuna dawa iponyayo.

²³ Kama nikikata mkono wangu, na nianguke hapa na kufa, unaona. Kama ungenipeleka kwa daktari, na—na kusema, “Waweza kumponya mtu huyu?”

Yeye angesema, “Mbona, amekufa.”

²⁴ Vema, ndipo unasema, “Hebu tuushone. Na nyinyi mna dawa fulani itakayoponya mkono huo, sivyo?”

“La, hatuna.”

²⁵ Unaona, kama wakinishona, na kunipatia mafuta ya kufanya maiti isioze ambayo yangenifanya nionekane wa asili kwa miaka mia moja, na kunidunga sindano ya penisilini kila siku, na kuweka dawa yote mahali hapo, hakika usingepona. Kwa nini? Kwa sababu kwamba uhai umetoka ndani yake.

²⁶ Vema, basi, ni gani mponya, dawa au uhai? Sasa wewe niambie kile uhai ulicho, na mimi nitakuambia kuwa Mungu ni nani. Unaona? Mungu ni uhai. Unaona? Wewe ni . . .

²⁷ Tulisema jana usiku, “Tuna wingi sana wa mitambo, na si nguvu tendaji.” Sasa, mwili wangu ndio mitambo, lakini mwili wangu hautafanya kazi pasipo na nguvu tendaji, roho. Unaona? Na roho huendesha mwili wangu, huuongoza.

²⁸ Kama mo—motokaa bila ya petroli ndani yake, bila ya nguvu za kuitia moto, unaona. Haijalishi jinsi nguvu tendaji zilivyo nzuri, ama ninamaanisha . . . mitambo imewekwa sawa, silinda, ninii . . . na po—pointi na plagi, na chochote zaidi, lazima iwe na umeme pia. Huna budi kuchukua hizo pamoja.

²⁹ Hivyo ndivyo Mungu alivyo. Ni sharti ichukue nwaminio pamoja na Mungu, kufanya muungano, ndipo jambo fulani linaenda kutukia.

³⁰ Kwa hiyo uponyaji wa Kiungu ni kama tu wokovu. Hakuna mtu anayehubiri Injili ya wokovu kwa ajili ya nafsi yako angetaka kuitwa mwokozi wa Kiungu, bali yeye angekuwa tu Mwokozi wa Kiungu sawa na mtu yeyote angekuwa anahubiri uponyaji wa Kiungu angekuwa mponyaji wa Kiungu. Kwa sababu, mtu huyo hawezi kusema angeweza kuokoa mtu, maana

Yesu tayari amefanya hivyo. Unaona? Vema. Bali, kwa kuhubiri kwake, yeye huwaelekeza kwa Kristo Ambaye ndiye Mwokozi.

³¹ Uponyaji wa Kiungu huwaelekeza tu kwenye kazi iliyomalizika ya Kalvari, “Kwa kuwa Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa mapigo Yake sisi tulipona.” Unaona? Unaona? Uponyaji wa Kiungu si kitu ambacho mtu fulani anacho, ambacho anaweza kuweka juu yako. Ni kile ambacho imani yako ilicho katika kazi iliyomalizika.

³² Ikiwa Yesu alisimama hapa usiku wa leo amevaa suti hii, ambayo Yeye alinipa, asingeweza kukuponya. Yeye angeninii tu... Yeye—Yeye huenda... Huenda ukajua kwamba ilikuwa ni Yesu; bali Yeye asingeweza kukuponya, kwa sababu Yeye amefanya hivyo tayari. Unaona, ingekubidi kuamini hilo. Sasa Yeye angesema, “Mtoto Wangu, hujui kwamba kwa mapigo Yangu wewe ulipona?” Unaona, Yeye amefanya hivyo tayari. Tayari ni kazi iliyomalizika. Ni wakati uliopita. Tunaliamini tu sasa. Basi, kwangu mimi, Neno lingetosha. Kama ulimwambia mtu fulani jambo fulani, hawakutaka kuliamini, vema, hilo—hilo lingetosha, acha waendelee na wasiliamini. Bali huyo si Mungu, unaona.

³³ Ni kama tu wimbo mdogo niliokuwa nikimsikia mhudumu na mke wake wakiimba, “Si kama wanadamu wanavyosameheana. Yesu husamehe na kusahau.” Unaona? Hatuwezi kusahau hilo, bali Yeye anaweza. Yeye ni Mungu. Yeye anaweza kusahau hilo; kamwe halikuwa. Aliweke katika Bahari ya Usahaulifu, na hata asilikumbuke. Yeye ni Mungu. Anaweza kuliondoa kutoka kwa kumbukumbu Yake kabisa. Lakini sisi hatuwezi kufanya hilo, unaona. Yeye anaweza.

³⁴ Sasa wakati ukimwamini Yeye, kwamba Yeye amekufanyia hili, “Alikuponya wakati Yeye—wakati Yeye alipojeruhiwa kwa makosa yako, na kwa mapigo Yake wewe uliponywa,” wakati uliopita. Sasa kitu cha pekee kikupasacho kufanya ni kuliamini. Sasa Neno hufundisha hilo. Hakuna mtu awezaye kusema kuwa Neno halifundishi hilo. Na Hilo hulifundisha, sasa, na sisi tunaona ushahidi mwingi sana wa watu wanaoponywa kila mahali. Bali kuna uponyaji wa Kiungu.

³⁵ Sasa kama ingekuwa wewe au mimi, kama tulituma neno letu, na mamlaka kama Mungu, vema, kama watu hawakutaka kuamini hilo, isingewabidi kuamini; hata hivyo, ni wao ndio wagonjwa. Bali si Mungu.

³⁶ Yeye pia aliweka Kanisani, mitume, manabii, walimu, wachungaji, na wainjilisti, unaona, yote hayo kwa ajili ya kukamilisha Mwili. Na katika Mwili huu, kila mwili wa mahali maalum, Yeye alitoa karama tisa za kiroho, nazo karama hizo ni—ni za aina tofauti; hekima, maarifa, kunena katika lugha, karama za uponyaji, kutafsiri lugha, na kadhalika; karama tisa za kiroho, zote kuonyesha upendo Wake kwa Kanisa, unaona,

kwamba Yeye anataka wewe ukae katika utaratibu, Roho Mtakatifu mkuu Mwenyewe akiwa ndiye Mwalimu wa Kanisa. Ni vibaya sana tulichukua askofu badala ya Roho Mtakatifu, kuwa mwalimu wetu, unaona. Bali sisi—sisi. . . Roho Mtakatifu ndiye Mwalimu ambaye Mungu alilipa Kanisa, kulikuza Kanisa, kulikuza katika onyo la Mungu. Kwa hiyo Roho Mtakatifu huweka karama hizi kwa njia huru Kanisani, nazo zinafanya kazi kikamilifu, ikiwa hutasisimkwa tu na kujaribu tu kuchukua kile unachofikiria mwenyewe.

³⁷ Hapo ndipo watu hufanya makosa. Ninakuta miongoni mwa watu, kwamba mtu fulani anashawishika kabisa na kwa namna fulani kuchochewa kidogo, na Roho Mtakatifu. Ambalo, ni ajabu, kuchochewa. Bali hapo mtu fulani atakuja kwako na kusema, “Hivi Bwana anasema *hivi-na hivi?*” Unaona, wewe—wewe haikubidi kuwapa jibu. Usiliseme isipokuwa Mungu analisema, ndipo una BWANA ASEMA HIVI. Ndipo hakuna kitu kiwezacho kulizuia lisitendeke. Halina budi tu kutukia.

³⁸ Ninampa mtu yeyote cha—changamoto, usiku wa leo, hujasikia Roho Mtakatifu akinena katika mikutano, kuhusu BWANA ASEMA HIVI, ila kwamba lilitendeka hivyo hasa, hakika, kutoka kwa mamiliononi ya visa. Unaona, Hilo kabisa halina budi kuwa kweli.

³⁹ Iwapo Roho Mtakatifu angekuja usiku wa leo na kuniambia, kwa ono, “Ninataka uende kwenye makaburi ya Marais, kesho, ninaenda kumfufua George Washington,” Ningealika ulimwengu kuja na kuliona likifanywa. Ingebidi ifanyike, unaona, kwa kuwa Roho Mtakatifu alisema hivyo. Hiyo hulifanya kweli.

⁴⁰ Lakini mpaka Yeye aseme hilo, wewe ngojeka tu, unaona. Unaona? Unajua umeokoka na unajua umejazwa na wema Wake. Pia unajua vile, Yeye akiwa ndani yako, Yeye atatimiza maisha Yake ndani yako. Kwa hiyo ridhika tu. Anataka kukutumia, hakika Yeye atafanya hivyo, unaona. Yeye anajua mahali ulipo.

⁴¹ Na mimi nafikiri, katika kufanya hilo kwa upendo na ushirika mmoja na mwenzake, tunasahau makundi haya yote, madhehebu na vizuizi, na jeshi kuu la Mungu huenda likipiga hatua taratibu kuelekea kwenye ushindi.

⁴² Ninaenda kusoma sehemu ndogo ya Maandiko, usiku wa leo, na wengi wenu huenda wakataka kusoma pamoja nami. Kama unataka kufanya hivyo, mbona, hakika unaweza. Na sasa tunataka kugeukia kwenye Kitabu cha Mathayo Mtakatifu, mlango wa 12, kama ungetaka kusoma pamoja nami ninaposoma. Katika kifungu cha 38, cha Mathayo Mtakatifu mlango wa 12.

⁴³ Na ninataka kutangaza sasa kile kilicho somo ambalo ninataka kuzungumzia ni: *Ishara Ya Wakati Huu*. Hili ni fungu dogo linalojulikana, na ninazungumza tu hili kwa sababu

nimekuwa nikiomba. Pia si—sipendi kuondoka juu ya mahubiri magumu na halafu nirudi kwenye mkondo huo tena. Kwa sababu, mtu yeyote anajua, kwamba karama za Roho Mtakatifu, hufanya kazi kwenye mkondo fulani. “Zipo karama za uponyaji, kwa Roho yuyo huyo; karama za lugha, kwa Roho yuyo huyo,” mkondo mwingine tu, na wewe unajivuta mwenyewe kutoka mmoja hadi mwingine. Kwa hiyo hebu tusome sasa. Kama wewe...

Kulikuwepo hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.

Bali akajibu akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakitapewa ishara—hakitapewa ishara yoyote, ila ishara ya nabii Yona.

Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.

Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

⁴⁴ Tunakuta hapa kwamba Bwana wetu, katika Maandiko ambayo ndiyo kwanza tusome, hilo lilikuwa katika mkondo wa kile Wayahudi wanaamini. Wayahudi waliamini ishara. Na hao walimjia Yesu, hawa wanatheolojia, na walikuwa wakihojiana na Yeye, kwamba wangetaka kuona ishara kutoka Kwake. Sasa unaona jinsi walivyokuwa vipofu? Yeye tayari alikuwa ameonyesha ishara Yake, kwamba kile alichokuwa Yeye, kwamba Yeye alikuwa Masihi.

⁴⁵ Tulikuwa kwenye hilo jana jioni. Ni wangapi waliokuwa hapa jana jioni? Hebu tuone. Hilo ni jema. Vema.

⁴⁶ Tulikuwa kwenye hilo jana jioni, na kuthibitishia wasikilizaji, kwamba ishara ya Masihi ambayo Yeye alipaswa kuonyesha, kwamba Yeye alikuwa ndiye Nabii yule ambaye Musa alisema angeinuka. “Na wote ambao hawakumwamini Nabii huyu, watakatiliwa mbali kutoka miongoni mwa watu. Bwana Mungu wenu atainua Nabii kama Mimi.” Ndipo wakati Yeye alipokuja na kufanya ishara ya Nabii, vema, wengi wao walitaka kusema kwamba yeye alikuwa Be—Beelzebuli au roho fulani mwovu.

47 Ndipo Yeye akawaambia, kasema, “Sasa, hili, hili mtasamehewa. Bali ajapo Roho Mtakatifu, na unene dhidi ya Huyu akifanya kazi ile ile, bila shaka, hutasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu au katika ulimwengu ambao unapaswa kuja.”

48 Sasa tunataka kuendea mambo haya si tu kwa wepesi, hatuna budi kuja kwa unyofu kwenye hili na kuona. Yesu alitoa tamshi hilo, kwamba wakati Roho Mtakatifu ajapo kufanya kazi ile ile ambayo Yeye alifanya, kwamba kusema neno moja dhidi Yake, hakutasamehewa kamwe katika ulimwengu au katika ulimwengu ujao.

49 Sasa, kumbukeni, Roho Mtakatifu hakutolewa hadi Pentekoste. Nao Wayahudi walikuwa tayari wameshuhudiwa na Mwanadamu Yesu Kristo; Wasamaria walikuwa wameshuhudiwa na Utu wa Yesu Kristo. Kwa hiyo Mungu mwenye haki asingaliweza kuwahukumu watu wenye haki, hapana budi kuwepo na watu wasio haki kwa ajili ya Mungu kuhukumu. Vema, basi, huyu Roho Mtakatifu hana budi kurudi katika siku za mwisho juu ya kanisa na kuonyesha ishara zile zile kama Yeye alivyofanya wakati ule, kwa sababu Mungu kamwe habadilishi njia Yake.

50 Mungu kamwe hafanyi jambo moja kwa njia *hii*, na njia nyingine afanye jambo jingine kwa njia tofauti. Unaona, uamuzi Wake wa kwanza ni mkamilifu kwa sababu Yeye ni Mungu. Unaona? Neno Lake haliwezi kubadilishwa. Yeye—Yeye—Yeye hakujifunza zaidi katika miaka hii elfu sita tuliyo nayo ya historia ya binadamu. Hakujifunza zaidi ya Yeye alivyofanya huko nyuma, kwa sababu Yeye hana kikomo kwa kuanzia. Unaona? Na Yeye kamwe habadilishi Neno La—La—Lake. Yeye hana budi...

51 Alichagua kumwokoia mwanadamu kwa Damu iliyomwagika ya yule asiye na hatia. Tumejaribu kuwaelimisha, tumejaribu kuwaundia dhehebu, tumejaribu kila kitu ulimwenguni, na maisha ya jamii, na imeshindwa kila sehemu, na itaendelea kushindwa mpaka tutakaporudi chini ya Damu. Hapo ndipo mahali pekee palipo na ushirika.

52 Mungu kamwe habadiliki. Mungu anaposema jambo lolote, hilo halina budi kubaki daima. Ikiwa Mungu... Kama mwanadamu alimjia Mungu, na Mungu akamponya mtu huyo juu ya msingi wa imani yake, inambidi kumfanya mtu anayefuata vivyo hivyo, ama Yeye alikosea wakati Yeye alipomponya mtu wa kwanza. Ikiwa Yeye alimwokoia mtu chini ya Damu, na Hiyo pekee, na atamwacha mtu fulani aingie tu chini ya elimu au kuwa mwanatheolojia fulani, au kitu fulani, pasipo Damu iliyomwagika kuwekwa kwake, Yeye alikosea wakati Yeye alipohitaji Damu kwa ajili ya mtu wa kwanza.

Unaona, Yeye hana budi kubakia vile vile. Kusudi Lake daima limekuwa lile lile. Matendo Yake daima yamekuwa ni yale yale.

⁵³ Hakuna wakati hata ambapo Mungu aliwahi kuhusika na dhehebu. Ichunguze katika historia. Yeye daima huhusika na mtu mmoja, kamwe si kikundi; mtu mmoja. Tunaona katika historia, kwamba wakati watu mashuhuri walipoinuka, Bwana aliwatuma jukwaani, na wakati walipoondoka, waliunda dhehebu nyuma yao. Na kamwe hakujawahi kuwa na wakati ambapo watu waliwahi kuunda dhehebu ila ambapo dhehebu hilo lilikufa, na kamwe halikurudi tena kwenye milki za kiroho kama lilivyokuwa. Ndio kwanza—ndio kwanza nimalize kupitia miaka ishirini ya historia ya Biblia, kwa hiyo hakuna mahali ambapo waliwahi kuinuka tena.

⁵⁴ Mungu hufanya kazi kwa ajili ya leo hii. Kile Yeye anachofanya kesho ni juu Yake. Na Yeye daima huhusika nasi, na mtu binafsi, unaona, maana makundi ya wanadamu yana mawazo mengi kupita kiasi.

⁵⁵ Angalia, hata mitume, baada ya wao kujaribu kuchagua mmoja, kwa sababu ya Yudas kuanguka, walipiga kura na ikamwangukia Mathiya. Hicho ndicho kilichokuwa kizuri kuliko vyote walivyoweza kufanya na funguo za Ufalme. Na hakuna Andiko lililoandikwa ambapo alifanya chochote. Bali Mungu alimchagua Sauli, maskini jamaa mwenye hasira kali, lakini ilimbidi Yeye kumwanguka kwa mgongo wake siku moja na—na kumfanya atazame juu kwa kitambo. Ndipo Yeye akasema, “Nitamwonyesha mambo makuu yanayompasa kuteseka kwa ajili Yangu.” Unaona? Unaona, kanisa lilimchagua Mathiya, bali Mungu alimchagua Paulo. Unaona, hiyo ndiyo tofauti. Mungu daima hufanya chaguo Lake, uteuzi Wake. Mungu hufanya hilo kwa uteuzi, kwa kujua Kwake kimbele.

⁵⁶ Sasa tunaona kwamba Mungu daima alihusika na watu, kwa ishara na maajabu. Ameahidi ishara za siku za mwisho. Mungu hawezi kubadilisha sera Yake. Yeye daima huwazungumzia watu kupitia manabii Wake. Kumekuwa na wakati mwingi, kote kupitia nyakati; bali Mungu daima alikuwa na nabii mahali fulani ambaye Yeye aliweza kuzungumza naye, kila mmoja ambaye Neno la Bwana lingeweza kumjia, na huyo pekee, unaona, juu ya nabii huyo. Unaona?

⁵⁷ Daima wangeenda chini na kutafuta kujua mahali nabii huyu alipokuwa. *Mwonaji* maana yake—*mwonaji* maana yake ama ni “kubashiri au kunena,” yeye ni mwonaji ambaye huona mambo yanayoenda kutukia. Na yeye hulibashiri kwa watu. Nayo Biblia ilisema, “Isipotimia, basi msimsikie.” Inabidi iwe ni kila wakati. Mungu hawezi kushindwa, unaona. “Na isipotimia,” basi Yeye alisema, “Yeye hakuwa na mtu huyo.” Kwa hiyo juu ya hilo, watu walijua kwamba Neno la Bwana lilikuwa pamoja

na huyu mwonaji ambaye Yeye alikuwa naye, waonaji wa Agano la Kale.

⁵⁸ Sasa Roho Mtakatifu habadilishi mkondo huo. Yesu alisema, “Wakati Yeye Roho Mtakatifu atakapokuja juu yenu, Yeye atawaonyesha mambo haya niliyowafundisha, nimewaambia, na Yeye atawaonyesha mambo yanayopaswa kuja.” Unaona, Yeye kamwe habadilishi mfumo Wake; daima ni ule ule, hivyo basi tunaweza kumtumainia Yeye.

⁵⁹ Lakini, unaona, sehemu zetu za kibinadamu hutufungamanisha kabisa katika mambo mbalimbali, na makundi ya wanadamu huungana pamoja na kupiga kura juu ya *hili* na *lile*. Hicho hapo ndicho kitu ambacho hututupa nje ya mstari, unaona, na kusema, “Vema, Hili lilikuwa ni kwa ajili ya siku nyingine.” La. Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Na Neno lote limevuviwa, yote ya Hilo.

⁶⁰ Sasa Yesu alikuja hasa katika ishara ambayo ilikuwa imfuate Yeye, kama Musa alivyotabiri kwamba Masihi atakuwa ni Nabii mpakwa mafuta ambaye Bwana atamwinua, na Yeye alikuwa ameonyesha wazi kwamba Yeye alikuwa ndiye huyo Nabii. Na sasa Mafarisayo hawa walikuja Kwake na kusema, “Mwalimu, twataka ishara kutoka Kwako.”

⁶¹ Akasema, mahali pamoja Yeye alisema, kama ungetaka kulisoma, katika Mathayo Mtakatifu mlango wa 16 na kifungu cha 3, 1 hadi 3, walimwuliza Yeye tena ishara. Na Yeye akasema, “Enyi Mafarisayo vipofu, wanafiki, mnaenda nje na kuona jua likitua,” na kasema, “nyinyi—nyinyi mnasema, ‘Kesho kutakuwa shwari.’ Kama ni kwekundu kidogo na kumetanda, mnasema, ‘Itakuwa hali mbaya ya anga.’” Kasema, “Enyi wanafiki, mnaweza kutambua uso wa anga; bali ishara ya wakati, hamwezi kutambua.” Walipaswa kuijua.

⁶² Sasa, sasa ikiwa huyu Roho Mtakatifu ajaye katika siku za mwisho inabidi awe hasa Uhai wa Kristo katika Kanisa, unaona, na ulimwengu unaomcheka Huyu ama kusema neno moja dhidi Yake, kwa mamlaka ya Neno la Mungu, utaangamizwa. Kwa hiyo unaona kile ulimwengu umefanya, kwa hiyo Mungu kunyesha hukumu kutoka mbinguni kuko katika utaratibu kabisa sasa hivi. Taifa letu, majiji yetu, ulimwengu wetu, umeiva kwa ajili ya hukumu.

⁶³ Na nina hakika kwamba kumechelewa kuliko tunavyofikiria. Alisema ingembidi Yeye kuufupisha kwa ajili ya Mteule, la sivyo hakuna mwanadamu atakayeokolewa.

⁶⁴ Wazia tu kuhusu kile, siku baada ya siku, mwaka baada ya mwaka, kinakuwa kibaya zaidi. Watazame watu wenu wa utakatifu, watu wa Kipentekoste, jinsi uozo umeingia ndani miongoni mwa makanisa; kuzozana, kukiendelea.

⁶⁵ Waangalie wanawake wetu. Ilikuwa ni kosa kwao kunyoa nywele zao; Biblia inasema, “Ni kosa.” Lakini wanafanya hata

hivyo. Ni, Biblia ilisema kwamba wasifanye hivyo. Na kuvaa nguo hizi ambazo huonekana kama nguo za wanaume; Biblia ilisema, “Hilo ni chukizo kwa Mungu.”

⁶⁶ “Loo,” unasema, “hao ni Wamethodisti.” Hao ni Wapentekoste. Hiyo ni kweli. Ni wote, unaona.

⁶⁷ Ni kwa nini? Mnapenda vipindi vyenu vya televisheni kuliko mnavyojali kuhusu kusoma Biblia. Unaona, mna—mnafanya watu hao mfano wenu badala ya Neno la Mungu. Unaona? Sasa, basi, inabidi iwe ni hukumu, na daima inazidi kuwa mbaya zaidi na zaidi.

⁶⁸ Sasa Yesu aliwaambia kwamba kutakuwa na ishara. Alizungumza kuhusu ishara za siku ya mwisho. Na jana usiku Yeye alituambia, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu, kwamba Roho wa Mungu angefunuliwa katika siku ya mwisho, katika mwili wa mwanadamu, ambaye ataweza kutambua mawazo yaliyoko moyoni, moyo.”

⁶⁹ Sasa Biblia inasema Neno la Mungu hufanya hilo, Waebrania 4, “Neno la Mungu lina nguvu zaidi, lina uwezo zaidi, na ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, hukata hata kugawanya, mafuta ya mfupa, na hutambua mawazo na makusudi ya moyo.”

⁷⁰ Hiyo ndiyo sababu, Yesu alikuwa ni Neno. “Hapo mwanzo,” Yohana Mtakatifu 1, “hapo mwanzo alikuwako Neno, Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Hiyo ndiyo sababu Yeye angeweza kuwaangalia na kutambua mawazo yao.

⁷¹ Hiyo ndiyo sababu Yeye aliweza kumwambia yule mwanamke kisimani, unaona, kwamba, “Umekuwa na waume watano.”

⁷² Hiyo ndiyo sababu Yeye aliweza kumwambia Fi—Filipo, wakati alipomleta Nathanaeli; Alimwambia Nathanaeli, “Tazama, Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

Akasema, “Ulinijua lini Wewe, Rabi?”

⁷³ Kasema, “Kabla Filipo hajakuita wakati ulipokuwa chini ya mti, nalikuona.”

⁷⁴ Mtambuzi wa mawazo, loo, sehemu nyingi sana katika Maandiko akijitambulisha Mwenyewe! Hiyo haikuwa kwa Mataifa. Hakuna wakati mmoja ambapo Yeye aliwahi kujitambulisha Mwenyewe kwa Mataifa namna hiyo. Yachunguze Maandiko. Hakuna hata wakati mmoja. Hiyo ni leo. Unaona? Mataifa walikuwa na miaka elfu mbili, ya masomo na theolojia; Yeye amechukua watu kutoka kwa Mataifa, kwa ajili ya Jina Lake; lakini sasa wakati umewadia ambapo hili halina budi kufanywa kabla tu ya kuteketezwa kama ilivyokuwa huko Sodoma.

⁷⁵ Huyu hapa alikuwa Yesu na ishara yake iliyotambulishwa, iliyothibitishwa, ishara ya Kimaandiko kwa watu, na hata hivyo hao Mayahudi wakisema, “Ningetaka kukuona Wewe ukifanya ishara.”

⁷⁶ Hivi umewahi kuwaona watu ambao ni wasioamini, watakuambia hilo, “Kama kukiweko, ninajua *fulani-fulani* huko mtaani, kama Yeye atawaponya!” Unaona? Loo, ni—ni . . . Unaweza kuona ni Shetani, kitu kile kile.

⁷⁷ Unajua walisema, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, shuka kutoka msalabani.” Wakafunga kitambaa kuzunguka kichwa Chake, kasema, “Jamaa huyu husema Yeye ni ‘Nabii.’” Wakampiga Yeye kichwani kwa kijiti, huku amefungwa kitambaa usoni Mwake, kasema, “Sasa tabiri na utuambie ni nani aliyekupiga Wewe,” wakati walipopitishana kijiti mmoja kwa mwingine, kasema, “tutakuamini Wewe.”

⁷⁸ Lakini, unaona, Mungu hamfanyii yeyote vitimbi. Yesu alisema, “Mimi hufanya tu kile ambacho Baba hunionyesha Mimi.” Unaona? Na hiyo ni kweli.

⁷⁹ Na huyo ni mtumishi wa kweli wa Mungu, daima ni mtiifu kwa Bwana wake. Unaona? Si kujionyesha ama—ama kusema jambo kumwinua mtu fulani mwingine, bali kuwa mwaminifu na mkweli na Yeye aliyemtuma. Huyu ndiye mtumishi wa kweli wa Kristo.

⁸⁰ Kama Elieza, mwakilishi, akitoka kwake Ibrahimu, unaona, kumchukua bibi-arusi kwa—kwa Isaka, Rebeka mrembo; mtiifu, mtumishi kielelezo, unaona, alikuwa katika shughuli za bwana wake, pekee. Ni mfano jinsi gani wa Roho Mtakatifu leo hii, kitu kile kile, akimchukua Bibi-arusi, unaona, katika wakati wa jioni ambapo nuru zinazimika.

⁸¹ Sasa walitaka kuona ishara. Ingawa Yeye alikuwa ametambulishwa, kikamilifu ishara za Kimaandiko, hata hivyo hawakutaka kuamini ishara ya Biblia. Walitaka Yeye afanye vitimbi. Hivi hamwoni? Hiyo ndiyo aina ile ile ya roho aliyesema, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yageuke kuwa mkate. Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, jitupe chini Mwenyewe kutoka hapa, maana imeandikwa Yeye atawapa Malaika Wake amri juu Yako; isije ikawa wakati wowote Wewe ujikwae mguu Wako kwenye jiwe, Hao watakubeba Wewe.” Bali Yeye hakuwa akijikwaa mguu Wake kwenye jiwe. Unaona? Hakika. Ndipo Yeye akasema pia hapo, kama ulitambua, wakati Yeye alipoweka huu juu ya msalaba, na kadhalika; sasa roho huyo hapa alikuwa ndani ya hawa Mafarisayo, akisema, “Sisi tunataka ishara.”

⁸² Akasema, “Kizazi kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara.” Tazama.

⁸³ Na Yeye, Mungu katika nyakati zote amekuwa na ishara kwa ajili ya watu Wake. Na pasipo kufanya chochote, Mungu hutuma

ishara, daima Yeye hutuma ishara kwanza. Na Yeye aliahidi Yeye angefanya jambo lilo hilo, maana Yeye hawezi kubadilika. Kwa hiyo tukiona wakati wa mwisho ukionekana, na ishara za wakati wa mwisho, hata ishara ya mwisho ambayo iliahidiwa kabla ya Sodoma kuteketezwa.

⁸⁴ Tumekuwa na furaha. Tumekuwa na nyo—nyota zikitikiswa mbinguni. Tumekuwa na vita, na uvumi wa vita. Tumekuwa na matetemeko ya nchi mahali mahali, na mambo hayo yote. Pamoja na, karama za Roho zimerudi kwenye kanisa. Tumekuwa na madhihirisho haya yote mbalimbali, ibada kubwa za uponyaji na kadhalika, zikionekana. Hizo zote ni ishara.

⁸⁵ Lakini ishara ya mwisho, kabla tu Mataifa kuteketezwa, ilikuwa ni ishara: Mungu akidhihirishwa katika mwili wa mwanadamu. Kweli. Na Yesu alisema hilo litakuwa kwenye kurudi Kwake. Tunapaswa kuwa waangalifu sasa na kuwa sawa hasa na Mungu. Kuwa na hakika kwamba uko sahihi, sasa.

⁸⁶ Walikuwa waninii, Wayahudi, daima walikuwa waegemea juu ya ishara zao, mnajua hilo, badala ya theolojia na hotuba. Iliwabidi kuegemea juu ya ishara, kwa sababu mwaminio halisi wa kweli daima anaamini kwamba Mungu ni Mungu wa uwezo.

⁸⁷ Na mahali Mungu alipo, ishara hazina budi kutokea. Unaona, ni kama tu kutwanga kipande cha chuma, moto, juu ya fuawe, unaona, cheche hazina budi kuruka. Inaakisi. Na kila mahali alipo Mungu, hapo pia, pana ishara na maajabu. Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” huduma kote ulimwenguni, unaona. “Ishara hizi zitafuatana nao,” daima ishara. Mungu daima hutoa ishara, kama Yeye alivyofanya mwanzoni, na huzitoa kwa kila kizazi, kwenye mwisho.

⁸⁸ Yeye alifanya hivyo wakati wa Nuhu. Nuhu alikuwa ni ishara kwa kizazi hicho. Alikuwa mlokole kwa macho ya ulimwengu. Kwa wanasayansi, mbona, ujumbe Wa—Wake kabisa haungeambatana na ufahamu wao wa kisayansi. Alisema, “Maji yanashuka chini kutoka mbinguni na yanaenda kugharikisha dunia.”

⁸⁹ Huenda wakaweza kurusha kwenye mwezi, ama kwa darubini yao, ama chochote kilichokuwa. Wakasema, “Hakuna maji huko juu. Ninaweza kuthibitisha kisayansi hakuna maji huko juu,” huenda wanasayansi walisema.

⁹⁰ Bali Nuhu akasema, “Mungu anaweza. Kama hakuna maji huko, Yeye ni Muumba, Yeye anaweza kuweka maji huko. Na Yeye anajua jinsi ya kufanya hivyo.” Lakini yeye alikuwa ni ishara. Aliendelea kujenga safina wakati hakukuwa na maji kwa ajili yake kuelea ndani, bali a—aliijenga hata hivyo. Alikuwa ni ishara kwa watu hao.

⁹¹ Vema, Musa alikuwa ishara katika Misri, wakati walipoona miujiza hii mikubwa, na kadhalika. Sulemani, na kuendelea.

⁹² Kisha tunapata hapa kwamba walimwita Yesu...ishara ambayo Yeye alikuwa anawapa, ishara ya kweli ya kinabii ya Maandiko yao.

⁹³ Sasa zipo ishara nyingi ambazo si ishara za Kimaandiko. Hatuna budi kuwa na ishara za Kimaandiko. Lazima ije BWANA ASEMA HIVI, kutoka kwenye Biblia hii, unaona, ndipo tunajua ni sahihi. Bila shaka, yapo mambo mengi sana ambayo huendana na hilo, kwamba Mungu anaweza kufanya chochote Yeye anachotaka kufanya. Yeye ni Mungu. Lakini ninajua Yeye hutimiza Neno Lake, kwa hiyo ninataka kuliona kutoka kwenye Neno Lake, ndipo ninajua ni kweli maana ni Neno.

⁹⁴ Sasa tunapata kwamba katika wakati huu, Yesu akionyesha ishara Yake ya Kimaandiko, na hata hivyo waliita ishara hiyo ya Kimaandiko...Kwa sababu hawakutaka kuamini hiyo kuwa ni ishara ya Kimaandiko, ilibidi wapate jibu kwa watu, kwa hiyo walisema, “Ni—ni akili Yake. Yeye—Yeye amepagawa pepo.” Na Yeye anaitwa, walimwita Yeye, “Beelzebuli.” Na Yeye alikuwa anawakemea kwa ajili ya hilo. Hilo litakuwaje wakati Yeye atakapokuja tena?

⁹⁵ Tazama, Yeye alimrejea Yona. “Kama ilivyokuwa katika siku za Yonas,” maana yake Yona, “ndivyo itakavyokuwa katika Mwana, kuja kwa Mwana wa Adamu.”

⁹⁶ Sasa watu wengi humhukumu Yona. Mimi simhukumu Yona. Unajua, wanasema, “Vema, yeye ni Yona.” Mmesikia msemu huo. Lakini hampaswi kufanya hivyo, enyi Wakristo. Hampaswi kuwahukumu watumishi wa Mungu. Yona alikuwa nabii. Hakuwa nje ya mapenzi ya Mungu. Alifanya tu hasa. Hana budi kufanya hilo kwa ajili ya ishara. Kila kitu hutendeka, si kwa kutendeka tu, hutendeka kwa ajili ya ishara.

⁹⁷ Wakati mmoja, ilibidi nabii amwoe kahaba, azae naye watoto. Mmoja alilala kwa ubavu wake kwa siku mia tatu na arobaini, kisha akageuka upande mwingine. Mmoja alivua nguo zake. Na kila kitu tu kilifanywa kwa ajili ya ishara, unaona. Naye Yona ilibidi afanye hilo kwa ajili ya ishara.

⁹⁸ Kumbukeni, Ibrahimu ilimbidi kumwoa Hajiri, kinyume na mapenzi yake mwenyewe, wakati Sara alipomkabidhi kijakazi, bali yeye alikataa hilo. Lakini Mungu akamtokea, kasema, “Msikie Sara, kwa sababu mwanamke aliye huru hatarithi pamoja na mwanamke mtumwa.” Ilimbidi kufanya mtoto huyo atupwe nje. Ilikuwa ni kitu gani? Ishara. Yote hayo ni ishara. Mungu hufanya mambo kwa ajili ya ishara.

⁹⁹ Naye Yona alikuwa ishara. Sasa ukitambua, Yesu analirejea hapa, “Kizazi dhaifu, kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara, nao wataipata. Kwa kuwa kama nabii Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na siku tatu usiku, vivyo hivyo imempasa Mwana wa Adamu, unaona, kuwa katika moyo wa

nchi siku tatu mchana na siku tatu usiku.” Yona alikuwa ni ishara ya nini basi? Alikuwa ni ishara ya ufufuo. Vema.

¹⁰⁰ Sasa, kama kuliwahi kuwapo na kizazi kilichopotoka, tunaishi ndani yake. Tunajua hilo. Kimepotoshwa, kiakili, kimwili, kijinsia, kila kitu. Kimepotoshwa. Kizazi kiovu, wasioamini, zaidi nadhani kuliko tuliowahi kuwa nao. Wao ni—wao ndio a—aina ya waaminio wa kikasisi, na hao ndio wagumu zaidi kushughulikia.

¹⁰¹ Mimi ni mmishenari. Nimesimama kwenye nyanja na kuona ambapo walileta makafiri, ambao hata hawakujua ni upi mkono wa kulia na wa kushoto. Wasingejua. Vema, a—anakuja katika hali yake. Kamwe hakusikia kuhusu Mungu. Sasa yeye anataka kuona kitu fulani. Na punde tu unapoweza kumthibitishia kilicho Kweli, atakikubali.

¹⁰² Lakini kafiri mwenye elimu; unaona, hilo ni neno baya kutumia, bali ni kweli. Unaona, kafiri mwenye elimu, yeye anataka kutoa wazo lake mwenyewe kuhusu hilo, unaona, yeye anajua mengi sana juu yake. Hawezi kujinyenyekeza kwa imani tu, kuangalia Neno la Mungu.

¹⁰³ Hivyo ndivyo hao Mafarisayo walivyokuwa katika siku hiyo, wasingeweza tu kuangalia Neno. Lilikuwa Hilo hapo, bali wao wasingetaka kuona Hilo. Na sehemu ya kuhuzunisha, kujua kwamba kwa hakika walikuwa vipofu. Mungu alifanya hilo kwa ajili ya ishara.

¹⁰⁴ Sasa angalia leo basi, ishara ambayo kizazi hiki kiovu ambacho tunaishi ndani yake kitaona, itakuwa ni ishara ya ufufuo. Yeye hakusema kutakuwa na “moja.” “Kizazi kiovu na cha zinaa chatafuta ishara, nao watapokea ishara ya Yona; ufufuo.” Na katika kizazi hiki kiovu, cha zinaa, kilichopotoka ambacho tunaishi ndani yake, ulimwenguni kote! Msifikirie mnacho chote katika New York. Hamna hao; hao wako kote ulimwenguni. Msifikirie Marekani ndiyo pekee iliyo na hao; hao wako kote ulimwenguni. Kweli. “Kizazi cha zinaa,” unaona, hao ndio wa kupokea ishara ya ufufuo.

¹⁰⁵ Katika siku hizi zote, ambapo tuna Buddha, Makalasinga, Wajaini, loo, kila namna ya dini, maelfu ya mifumo hiyo kote ulimwenguni, kila mmoja wao anaweza kukupeleka kwenye kaburi la waanzilishi wao. Bali Ukristo una kaburi tupu. Unaona?

¹⁰⁶ Si hayo tu, bali huwezi kuwaambia hao watu, useme, “Yeye anaishi moyoni mwangu.” Watakurudisha moja kwa moja kwenye Neno Lake. Hakika watakurudisha. Watakurudisha moja kwa moja kwenye Neno Lake. Naam. Huwezi kutoa saikolojia kwa—kwa kafiri, unaona, kwa sababu mungu wake anaishi moyoni mwake, pia.

¹⁰⁷ Niliwaona Waislamu wakilala mtaani, na kusema, “Allah, allah,” mpaka wanapagawa sana hata wangeweza kuchukua

kipande cha—kipande cha kibanzi na kukipitisha katika vidole vya—vyao, kamwe hawahisi.

¹⁰⁸ Niliona mwanaume huko Zurich, Uswisi, akichukua upanga na kuupitisha moja kwa moja kwenye mapafu yake, namna hii, na kuupitisha moja kwa moja. Na walikuwa na daktari aliyekuja jukwaani, na kumimina maji kupitia mahali ambapo upanga, ulipitia ule mwingine. Akauchomoa, na hata hatokwi damu. Unaona? Wanachukua kibanzi na kukichomeka kupitia kidevu chao, na juu kupitia pua yao.

¹⁰⁹ Sasa, afadhali ujue kile unachozungumzia wakati unapoenda kuzungumza kuhusu Mungu kwa mtu kama huyo. Afadhali ujue. Saikolojia tu haitafanya kazi. Atakufanya ujue hilo upesi sana. Inakubidi kujua kile ambacho unazungumzia.

¹¹⁰ Lakini kumbukeni Mungu aliyekuwa pamoja na Eliya juu ya Mlima Kameli, Yeye angali Mungu leo vile vile tu. Na mimi nimemwona Yeye mbele za mamia ya maelfu hasa ya watu, akilifanya; unaona, kuona waganga, kwa wingi, wakisimama hapo na kukupa changamoto, na kumwona Roho Mtakatifu kile ambacho Yeye hufanya. Unaona? Mmesoma vitabu na mnajua; na kutia sahihi taarifa za kile Mungu afanyacho. Yeye angali ni Mungu. Yeye anawajibika kwa Neno Lake. Sasa, Yeye hawajibiki kwa shauku zako. Yeye anawajibika kwa Neno Lake Mwenyewe. Unaona? Sasa tunaona hapa hawa makafiri, jinsi ambavyo wangepanya.

¹¹¹ Sasa Mungu katika siku hizi za mwisho aliahidi kwamba Yeye angeonyesha, kizazi kiovu na cha zinaa, ishara ya kufufuka Kwake, kwamba Yeye hajafa. Yu hai. Yeye hutimiza kila Neno, Yeye huliishi moja kwa moja kupitia wewe. “Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena,” alisema Yesu, “hata hivyo nyinyi mtaniona,” unaona, akizungumza na mwaminio, “kwa kuwa Mimi,” Mimi ni kiwakilishi cha nafsi, “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa ulimwengu, ukamilifu.” Nazo kazi, Yohana Mtakatifu 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye pia atazifanya.” Kazi zile zile! “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele,” Waebrania 13:8.

¹¹² Sasa kanisa limekuja kupitia wi—wingi wa nyakati za kanisa, baada ya ule wa kwanza, Wakati wa Kanisa la Efeso, katika Biblia. Na Bwana akipenda, kabla sijaondoka hapa, ninataka kuhubiri juu ya somo dogo liitwalo *Kuhesabu Kinyumenyume*, na kuona jinsi ambavyo tumekuwa, jinsi tumeendelea. Sasa angalia sasa kwenye Wa—Wakati wa Kanisa la Efeso na nyakati hizo za kanisa, mpaka ikaingia kwenye Wakati wa Giza wa miaka elfu moja ya giza. Ndipo basi Luther, akiwa ndiye mrekebishaji wa kwanza, alitoka na kuhesabiwa haki; hapa akaja Wesley, akiwa na utakaso; hapa wakaja Wapentekoste, wakiwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kanisa kila mara likiingia katika uchache, nguvu kuu zaidi. “Adui

anapokuja kama gharika, Roho wa Mungu atainua kiwango dhidi yake.”

¹¹³ Na sasa tumeuacha wakati wa Pentekoste. Sasa tunakuja kufikia mahali ambapo kama katika piramidi, si mafundisho ya piramidi sasa, bali ninamaanisha kama vile piramidi. Jiwe la kichwa wakati likija kutoshea, lazima lichongoke. Lazima kuwe na huduma ndani ya Kanisa, Kanisa la kweli la Mungu aishiye, ambapo wakati Jiwe la kichwa likija, Kristo, ama huduma ya Kristo, na Kristo watatoshea moja kwa moja pamoja kikamilifu. Halafu hilo linarudisha Waliokombolewa, kuipeleka Nyumba yote ya Mungu Utukufuni; Methodisti, Baptisti, na Presbiteri, kupitia nyakati kuu za marekebisho, waliotoka na kutoa maisha yao katika mateso na kadhalika kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Bali Jiwe hilo linakuja. Naam, bwana. Hakika litakuja. Mungu atalituma Hilo. Litatoshea Jengo lote pamoja juu yake. Unaona? Sasa tunaona ishara hizi, tunapoona huduma kutoka kwa Kristo ikianza kuwa nyembamba sasa, kwa huduma kamilifu ya Kristo, katika utimilifu wa Roho Mtakatifu.

¹¹⁴ Chini ya Luther ilikuwa ni Roho Mtakatifu yule yule, kuhesabiwa haki; kisha utakaso chini ya Wesley; jumbe; halafu ubatizo wa Roho Mtakatifu, ikifanya tatu. Tatu, si hatua tatu za neema, bali vituo vitatu, huenda nikaviita.

¹¹⁵ Tazama namna hii. Mtoto anapozaliwa, kuna vitu vitatu vinavyofanya kuzaliwa kwake. Kitu cha kwanza katika uzazi wa kawaida... Enyi watu wazima sikilizeni kwa makini sasa; watoto wachanga hawatalishika. Lakini, hebu tuone, kitu cha kwanza katika uzazi wa kawaida ni maji, halafu damu, kisha uhai. Unaona?

¹¹⁶ Sasa hilo ni jambo lile lile ambalo hufanya kuzaliwa kupya; maji, Damu, Roho. Elementi zilizotoka katika mwili Wake ndizo hufanya Mwili Wake. Unaona? Ilitoka katika mwili Wake, ndiyo bidhaa ambayo inahitajika ku—kumfanya Bibi-arusi Wake. Kwa sababu, Adamu alikuwa na bibi-arusi wake kutwaliwa kutoka kwa mwili wake. Kristo ametwaliwa Bibi-arusi Wake kutoka kwa mwili. Na wakati Kristo alipokufa, kulikuwa na vitu vitatu vilivyotoka katika mwili Wake; maji, Damu, Roho; kuhesabiwa haki kupitia kuamini, maji; kutakaswa kupitia Damu; ubatizo wa Roho Mtakatifu.

¹¹⁷ Sasa hatua hii kubwa ya mwisho haina budi kuingia katika ukamilifu, kwamba Roho Mtakatifu inabidi aishi ndani ya Kanisa hilo kikamilifu sana, atafanya Kichwa na Mwili kuunganika pamoja. Unaona? Unaona? Huo ndio Mwili. Yeye ndiye Kichwa katika Mwili. Sasa tunaona kwamba Yeye aliahidi, katika siku hizi za mwisho, kwamba hilo lingefanyika. Tunaliona.

¹¹⁸ Sasa, Yona. Watu wengi, nimesema, kuhusu Yona, walisema, “Vema, jamaa huyo alikuwa asiyeamini.” La, hakuwa.

119 Alipaswa kuenda Ninawi, hiyo ni kweli kabisa, kwa sababu lilikuwa ni jiji kubwa lililojaa dhambi. Na labda watu nusu milioni ndani yake, na walikuwa wabaya sana, sana. Walikuwa ni jiji kubwa la biashara. Kazi yao kubwa ilikuwa ni uvuvi, nasikia, na ndivyo walivyokuwa. Alitumwa huko chini, lakini aliingia kwenye chombo kisichofaa na kuenda Ta—Tarshishi.

120 Sasa watu wengi hujaribu kusema kwamba hakutaka kufanya hilo. Ninaamini yote yalipangwa na Mungu. Nilikuwa nikisoma hadithi ndogo, huenda ikashuhudia kusema kwenye wakati huu, kwa namna fulani kumtetea Yona, kuingia katika kile ninachotaka kusema.

121 Sasa, Yona, alipopanda chombo kingine, kitu cha kwanza unajua, alikuwa anaelekea njia isiyofaa na wakaingia katika shida. Upepo ukaanza kuvuma, ma—mawimbi yakaanza kunguruma, na kila mtu akafikiria chombo kilikuwa kinaenda kuzama. Kwa hiyo Yona alikuwa amelala usingizi, ndipo wakasema, “Amka, Ewe mwenye kulala, na umwitie Mungu wako!”

122 Ndipo Yona akakiri kwamba alikuwa makosani. Alisema, “Sasa nyinyi nifungeni miguu yangu na mikono yangu, mkanitupe majini, na ndipo dhoruba itakoma.” Nao wakafanya hivyo.

Naye Mungu alikuwa ameandaa samaki mkubwa.

123 Sasa, nilimsikia mwanasayansi hapa si muda mrefu uliopita, huko Louisville, Kentucky; ambapo, nilikuwa nikiishi Jeffersonville, upande mwingine tu. Walikuwa na fremu ya nyangumi imewekwa juu ya—juu ya motokaa na jamaa huyu alikuwa akihutubu, huyu mwanasayansi, na kueleza ni meno mangapi aliyokuwa nayo, na, loo, sijui. Kwa hiyo basi hatimaye alisema, “Mnajua, ha—hadithi ya Biblia,” kasema, “ambayo si kweli,” akasema, “Biblia. . .”

124 Hilo lilizidi kabisa kwangu mimi, kwa hiyo nikapanda tu karibu kidogo. Nikawaza, “Ninaenda kuona kile anachoenda kusema.”

125 Akasema, “Hadithi ya Biblia ya—ya nyangumi kummeza Yona,” kasema, “ninawatakeni enyi watu kutazama. Mtu angeweza kupitia koo lake, wakati usingeweza hata kurusha mpira wa besiboli kupitia koo lake?” Kwa hiyo akasema, “Hilo ni kosa.”

126 Nisingeweza tu kusimama na kumwacha huyo kafiri kusema mambo kama hayo. Nikasema, “Samahani, bwana. Je! uliwahi kusoma Biblia?”

Akasema, “Hakika.”

127 “Vema,” nikasema, “halafu unatoa tamshi kama hilo? Mungu kamwe hakusema ilikuwa ni nyangumi. Mungu alisema alikuwa ni ‘samaki.’”

Akasema, “Vema, huyo angekuwa ni nyangumi.”

¹²⁸ Nikasema, “Kama ni, acha awe nyangumi. Alikuwa ni aliyeandaliwa maalumu, kwa kuwa Mungu aliandaa samaki kwa ajili yake.” Huyu alikuwa maalumu. Aliweza kutengeneza mmoja ambaye motokaa ingeweza kuingia ndani yake. Yeye ni Mungu, unaona, kwa hiyo hiyo ni kweli. Sisi, hatutaki kuamini hilo, mambo hayo, ama hadithi za Biblia. Mungu alimwandaa samaki huyu kwa ajili ya Yona. Alikuwa samaki maalumu, kwa hiyo a—alimmeza Yona.

¹²⁹ Na sasa yeye alikuwa chini katika tumbo la nyangumi. Na mikono yake imefungwa nyuma yake, na miguu yake imefungwa. Sasa unaweza kuwazia ni hali ya namna gani mtu huyo alikuwa ndani yake. Na, hata hivyo, nya—nyangumi, ama alikuwa ni kama samaki yeyote mwingine, labda, anaogelea kupitia kwenye maji mpaka anapopata chakula chake, na halafu anaenda chini kwenye sakafu ya bahari.

¹³⁰ Sasa wewe mlishe maskini samaki wako wa dhahabu na umwangalie. Anajaza maskini tumbo lake halafu anaenda chini kwenye sakafu ya bahari, na kutokeza maskini viogeleaji vyake. Na hapo anatulia, unaona, maana a—amepata chakula chake.

¹³¹ Vema, wakati samaki huyu alipokuwa amempata nabii, na alikuwa amemmeza, vema, basi lazima aliingia chini katika—katika sakafu ya bahari. Sasa, sijui kwamba aliingia, bali ninasema hu—hu—huenda alifanya hivyo. Na sasa huyu hapa mtu huyu.

¹³² Sasa sisi daima, ni vibaya sana, bali daima sisi hujaribu kuwazia, na kuonyesha, ama Shetani akituonyesha dalili zetu. “Vema, unaona, wewe, wewe si bora kuliko ulivyokuwa jana. Wewe, unaona, wewe si bora.” Usiangalie dalili.

¹³³ Kama mtu yeyote angekuwa na dalili, ingekuwa ni Yona. Unaona? Unaona, kila mahali alipotazama palikuwa ni tumbo la nyangumi. Unaona? Lakini unajua kile alichosema? “Ni ubatili unaodanganya.” Kamwe hakusema, “Ninaenda kuangalia kwenye *hii*.” Alisema, “Mara moja zaidi nitatazama hekalu Lako takatifu.”

¹³⁴ Kwa kuwa alijua, wakati Sulemani alipoomba na kuweka wakfu hekalu hilo, kasema, “Kama watu Wako wakiwa katika shida, popote, na kutazama mahali hapa patakatifu na kuomba, basi sikia kutoka Mbinguni.” Alikuwa na imani katika maombi ya Sulemani, mwanadamu, mwanadamu wa ardhini kama mimi na wewe, yeye baada ya kitambo hata alirudi nyuma, wanawake walimvuta mbali na Mungu. Na, bali, maombi yake yalisikiwa na Mungu, na aliweza kuwa na imani chini ya hali hizo.

¹³⁵ Na ni imani nyingi zaidi jinsi gani tunayopaswa kuwa nayo, wakati haitubidi kutazama hekalu lililojengwa na mwanadamu; bali Mbingu Yenye, ambapo Mwana wa Mungu ameketi

katika mkono wa kuume wa Ukuu Wake, na Damu Yake Mwenyewe, akiishi daima kufanya maombezi!

¹³⁶ Na hakuna mmoja wetu aliye na dalili aina kama hiyo. Tunaona watu wakiponywa katika Uwepo wa Mungu, wakati wote. Hatupaswi kamwe kutazama dalili; ni ubatili udanganyao. Mtazame Mungu, huyo Ndiye aliyetoa ahadi.

¹³⁷ Sasa tunaona kwamba chochote kilichofanyika, jinsi Mungu alivyompa oksijeni nabii huyo, mimi sijui. Lakini a—aliishi kwa siku tatu mchana na usiku, kulingana na Biblia. Na mimi sijui Tarshishi ilikuwa mbali kiasi gani, na ilikuwa umbali gani kutoka Ninawi, ni mbali kiasi gani walikuwa huko nje baharini; bali Yona alibaki hai, kulingana na Maandiko, kwa siku tatu mchana na usiku. Yeye alimwita.

Unasema, “Loo, hiyo haiwezekani.”

¹³⁸ Vipi kuhusu kumwita Lazaro, baada ya kuwa amekufa kwa siku nne? Unaona? Na Yeye atatuita siku moja, ingawa tumekufa miaka elfu kumi. Haileti tofauti yoyote, unaona, itakuwa sawa. Unaona, Yeye ni Mungu.

¹³⁹ Sasa tunamkuta sasa, na yeye huyu hapa anakuja mpaka Ninawi. Nyangumi anakuja moja kwa moja kupitia majini, kama kumbeba kwenye teksi. Safari ya teksi chini ya bahari, akija moja kwa moja kufikia Ninawi, na hapana shaka ilikuwa yapata adhuhuri.

¹⁴⁰ Vema, sasa, watu hao walikuwa ni wavuvi. Na wao walikuwa nje wakivuta nyavu zao, na kadhalika, wavuvi wao wa kiuchumi. Nao walikuwa makafiri. Waliabudu sanamu. Na mmoja wa miungu yao. . .

¹⁴¹ Kama Wahindi walivyokuwa nayo hapa Marekani, dubu wa kijivu alikuwa ni mungu, Ovegus, ambaye alikuwa mungu aliyeabudiwa na Wahindi makafiri kabla ya wao kuletwa katika Ukristo. Walikuwa na mungu, mungu wa mamlaka.

¹⁴² Basi, huko Ninawi, ninaambiwa kwamba nyangumi alikuwa ndiye mungu wa bahari, kwa sababu yeye ndiye bwana wa bahari. Anaweza kumeza chochote. Na yapata wakati wa adhuhuri, huyu hapa anakuja mungu wao, anapanda juu kutoka baharini; anafungua tu kinywa chake, naye nabii anatoka akitembea moja kwa moja kwenye ufuo. Si ajabu waliamini, unaona. Unaona? Wao, hakika waliamini, kwa sababu nabii, aliyekuwa akitoa ujumbe, alitoka katika kinywa cha mungu wao, “Tubuni la sivyo jiji hili linaenda kuangamia.” Unaona?

¹⁴³ Kwa hiyo hakuwa nje ya mapenzi ya Bwana. Alikuwa anafanya tu, kama, “Mungu hufanya kila kitu kufanya kazi pamoja kwa wema kwa hao wanaompenda Mungu,” hiyo ni kweli, “na waliitwa kulingana na kusudi Lake.” Yesu alimrejea.

¹⁴⁴ Halafu mmoja zaidi kabla hatujafunga kwa ajili ya mstari wa maombi. Alirejea Sulemani pia.

¹⁴⁵ Sasa, wakati Mungu anapotuma karama duniani, na watu wanaiheshimu, daima ni wakati adhimu kwa watu hao. Lakini wakiikataa, daima ni machafuko kwa watu hao. Yeye—Yeye hufanya hivyo, kila wakati. Tazama tu. Tazama wakati walipomkataa Yesu, na wakati walipowakataa manabii, na kadhalika, kile kilichokuwa.

¹⁴⁶ Bali katika wakati wa Sulemani, waliamini, wote. Sulemani alikuwa na karama ya utambuzi. Mungu alimpa Sulemani hiyo. Hiyo... Na watu wakaiamini, wote kwa nia moja. Walikuwa—waliitwa u—utawala wa miaka elfu, karibu, kwa ajili ya jamii ya Waebrania kwenye wakati huo. Ulikuwa ni wakati adhimu, wakati wa Sulemani. Hapana vita wala chochote; Yeye aliufanya kunawiri. Walijenga hekalu na vitu hivi vyote vikubwa ambavyo walifanya kupitia wakati wa Sulemani, kwa sababu yeye alikuwa mfano, Mwana wa Daudi, unaona, Mwana wa kimwili wa Daudi. Sasa, tunakuta kwamba katika wakati huu, wakati walipojenga hekalu na kila kitu, kila mtu aliheshimu karama hiyo ambayo Mungu aliwapatia, na hata kumfanya mfalme wao. Na sifa ikaenea kila mahali.

¹⁴⁷ Ninawaambieni, Wamarekani, kama tungaliheshimu tu karama ambayo Mungu ametutumia, Roho Mtakatifu, isingalitubidi kuwa na wasiwasi kuhusu wanaanga wa Urusi na mabomu ya atomiki, na kadhalika. Vema, huo ndio usalama we—wetu, ni Kristo. Unaona? Yeye ndiye usalama wetu.

¹⁴⁸ Lakini shida yake ni kwamba, Yeye hututumia karama na sisi tunaicheka na kudhihaki, kama tu walivyofanya. Hiyo ndiyo sababu tunaelekea hukumuni. Tuna... lazima iingie. Ni, tu, Mungu hapendelei mtu. Kama Mungu angaliacha ulimwengu huu uepuke, hii New York, hii Marekani, ulimwengu huu, uepuke na kile umefanya sasa, bila ya kuleta hukumu juu yake, Yeye angewajibika, kama Mungu mwenye haki, kuinua Sodoma na Gomora na kuomba msamaha kwa kuwateketeza, kwa kuwa Yeye aliwateketeza kitu kile kile ambacho sisi tunafanya sasa hivi. Unaona? Unaona? Kwa hiyo Yeye aliahidi ingekuwa hivi.

¹⁴⁹ Sasa tuliona sasa, kwamba katika siku za Sulemani, ungeweza kuwazia, kila mtu akizungumza kuhusu Mungu, "Loo, uwezo mkubwa wa Sulemani wa utambuzi!" Hiyo ilikuwa ni karama ambayo iliweza kutambua, na kila mtu alikuwa anajivunia kuhusu hiyo. Hakukuwa na mchafuko, kusema, "Ah, hapana, hapana!" Wote waliamini hiyo. Na sifa ikaenea kuingia kila mataifa. Na mataifa yakaogopa Israeli, bali si kwa sababu walikuwa na jeshi bora, bali kwa sababu Mungu alikuwa miongoni mwao. Hilo ndilo huleta hofu, Mungu. Mungu alikuwa miongoni mwao.

¹⁵⁰ Loo, jinsi inavyopaswa kuwa pamoja nasi, kukiri kuwa taifa la Kikristo! Ni vibaya sana kwamba madhehebu na kadhalika

yametusokota katika hali kama hiyo, kwa vile sote tuko nje ya utaratibu leo, na karibu hakuna mtu ajuaye kitu cha kuamini.

¹⁵¹ Basi, tazama, ndipo umaarufu wa Sulemani ukaenea kote kuingia Sheba. Malkia akausikia. Yeye alikuwa ni kafiri. Na kila, njia pekee waliyokuwa nayo wakati huo. . . Hawakuwa na televisheni na vitu tulivyo navyo leo hii, au magazeti. Njia pekee waliyokuwa nayo kutuma jumbe ilikuwa mdomo kwa sikio. Na kila wakati msafara ungeingia, hapana shaka maskini malkia angetoka nje na kusema, “Hivi mlipitia Palestina mlipokuwa mnateremka kuja huku?”

“Naam.”

“Je! ni kweli, kile wanachosema?”

¹⁵² “Loo, unapaswa kukiona! Hakuna kitu kama hicho! Watu hao wana uamsho huko juu. Wewe. . . Ni jambo la taifa lote. Loo, wana uamsho wa ajabu. Na Mungu wao amempaka mafuta mfalme wao, na yeye ana karama ya utambuzi. Na wewe hujawahi kuona chochote kama hiyo. Hakuna chochote kinachoweza kuzidi hekima hiyo. Yeye anaweza kutambua chochote. Ni—ni zaidi ya hekima ya mwanadamu. Ni utambuzi unaotoka kwa Mungu.” Na wao wote, mbona, walisikia.

¹⁵³ Unajua, “Imani huja kwa kusikia, kusikia Neno la Mungu.” Si kusikia kwamba sisi ni Methodisti, Baptisti, au Pentekoste; bali kusikia Neno la Mungu, unaona. “Imani huja kwa kusikia.”

¹⁵⁴ Na wakati wao, yeye angesikia, njaa iliingia. Vema, sasa, aliamua, baada ya yeye kusikia haya yote, kabla hajaweza kusema lolote juu yake, kwamba angeenda ajionee mwenyewe kabla ya kutoa maoni yake. Loo, hilo si lingekuwa zuri kama sote tungefanya hilo? Unaona? Ingawa hapana shaka kwamba alipitia magombo mengi, Biblia, ya manabii, ya kile walichokuwa wametabiri, kuona tabia ya Mungu wao Yehova.

¹⁵⁵ Sasa maskini malkia huyu alikuwa na mambo mengi kumkabili kabla hajaenda huko juu. Kitu cha kwanza, akiwa kafiri, ingembidi kwenda kwa kuhani wake, kuomba ruhusa, kwa sababu alikuwa ni malkia na mshiriki wa kanisa. Kwa hiyo ninaweza kumwazia yeye akienda juu kwa kuhani, na kusema, “Baba, je! ninaweza kuenda Israeli kupata hekima fulani kutoka kwa mtu huyu mashuhuri, Sulemani, ambaye Mungu wao ameweka hekima juu yake?”

¹⁵⁶ Ninaweza kumsikia akisema, “Mtoto wangu, kamwe nisingewazia kama hilo kutoka kwako. Dhehebu letu halishiriki katika uamsho huo.” Lakini unajua jinsi ingekuwa leo hii. Ninaifanya sasa kutoka kilicho bora zaidi hadi kilicho cha mzaha, bila shaka. Lakini sasa ingekuwa ni roho yule yule leo hii angesema hilo. Unaona, roho yule yule angeleta, kuifanya namna hiyo. Ndipo yeye. . . “Lazima usifanye hivyo, unaona. Kwa sababu, hata hivyo, watu hao ni. . . Hao ni walokole. Wanaamini kila namna ya ishara na vitu. Bali, vema, unaona,

kila mtu anajua kwamba hao ni kundi la walokole. Kama bahari zikikauka, na namna hizi zote za mambo ambayo wamekuwa nayo, hakuna moja la hayo lililo kweli. Unaona, ni hekaya tu ambayo imesimuliwa, ama wimbo ambao umeimbwa, au kitu fulani. Na hakuna kitu kwa hayo.”

¹⁵⁷ Lakini, unajua, wakati imani halisi inapogonga ndani ya moyo, wanaanza kuona njaa. Wanataka kuona.

¹⁵⁸ Hakuna mtu anayeishi ila ambaye angependa kuona zaidi ya wakati, pazia. “Nilitoka wapi? Mimi ni nani? Na ninaenda wapi?” Kati ya vitabu vyote vizuri ambavyo vimesomwa, chaguzi mashuhuri ambazo zimefanywa, kipo Kitabu kimoja tu ambacho hufunua kuwa wewe ni nani, mahali ulikotoka, na mahali unakoenda. Jambo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo. Na Hicho pia hutufanya tutazame kupita pazia, kuona.

¹⁵⁹ Sasa walipoona hili likitendeka, alisikia kuhusu hili, ndipo yeye akasema, “Nitaenda kwa vyovyote vile.” Kwa hiyo haijalishi kile askofu asemacho, ama chochote kilichokuwa, anaenda kuenda kwa vyovyote vile, amekusudia, kwa sababu anataka kuona kitu halisi, kitu fulani.

¹⁶⁰ Vema, ndipo kuhani labda alimwambia, kasema, “Sasa angalia, binti yangu, wewe ni malkia, hupaswi kushirikiana na watu kama hao.”

“Haijalishi, mimi ni mwanadamu ambaye hana budi kufa, pia.”

¹⁶¹ “Vema, sasa, kama kulikuwa na chochote namna hiyo kikiendelea, kingekuwa moja kwa moja hapa katika kanisa letu.” Bila shaka, roho huyo hajafa pia, unaona. “Hiyo, inabidi ije kupitia letu, la siyo si sahihi.”

¹⁶² Vema, huenda alisema, “Nimekuwa hapa tangu nilipokuwa msichana mdogo, aliyewekwa wakfu. Nimeona sanamu hizi zote na vinyago, na kadhalika, na wewe umenena kuvihusu kuwa ni miungu. Nyanya yangu alikuwa mshiriki hapa, na nyanya wa mama yangu, na nyanya wa nyanya wa mama yangu. Na hakuna hata mmoja wao aliyeonyesha chochote, ishara yoyote ya uzima. Wanasema kwamba Hiyo ni ‘Uzima.’”

¹⁶³ Kunapaswa kuwa na watu wengi zaidi wenye wazo la aina hiyo kama malkia alilokuwa nalo, papa hapa katika New York na kote ulimwenguni.

¹⁶⁴ “Ninataka kujionea hilo, mwenyewe. Na mimi sioni sanamu hizo. Ninakusikia ukisoma namna zote za vitabu, na vitabu vya sala, na kadhalika, lakini ni nini hicho? Sioni msogeo wa chochote kilicho hai. Vyote vimekufa, theolojia fulani au kitu fulani. Moyo wangu unatamani kuona. Ni wapi alipo Mungu? Yuko wapi?”

¹⁶⁵ Loo, laiti ulimwengu ungetamani hiyo! Yuko wapi? Kama Yeye aliwahi kuwa Mungu, Yeye angali inabidi awe ni Mungu.

Kama Yeye hakuwa, Yeye alikufa. Unaona? “Yeye ni yule yule,” Biblia ilisema, “jana, leo, na hata milele.”

¹⁶⁶ Sasa tazama, moyo wake unaanza kuona njaa sasa, kwa hiyo alikuwa na wazo jema. Alisema, “Ninaenda kuchukua kiasi fulani cha fedha, na ubani na kadhalika, manemane. Na kama kitu hicho ni sahihi, ninaenda kukiunga mkono. Kama si sahihi, nitaachana nacho.”

¹⁶⁷ Kwa hakika yeye angeweza kuwafundisha Wapentekoste! Kuunga mkono kitu ambacho kinakuita mtakatifu anayejibingirisha na kila kitu kingine, unaona, na bado unakiunga mkono. Unaona? Loo, jamani! Na karama ya hekima inapaswa kuwa ndani ya kanisa. Sasa tazama. Hiyo ni kwa ajili ya wachungaji kusema. Sasa tazama.

¹⁶⁸ Ndipo anasema hivi, “Nitazibeba zawadi zangu pamoja nami. Na ikiwa si kweli, ninaweza kurudisha zawadi zangu.” Hilo ni jema. Sasa maskini mama huyo akawa tayari kuenda. Akachukua matoashi wachache, fedha hizi zote, na wajakazi wake.

¹⁶⁹ Sasa wazia tu umbali uliombidi kusafiri, kuona kama hiki kilikuwa sahihi au sivyo. Unaona? Ipime kwenye ramani yako, kutoka Palestina kuteremka mpaka Sheba. Ni siku tisini kamili, miezi mitatu juu ya mgongo wa ngamia. Hakuninii. . . Alikuwa na ugumu. Asingeweza kuja katika Kadilaki iliyoyoyozwa kama sisi tufanyavyo. Bali, yeye, alikuja kutoka pande za mwisho wa ustaarabu, ulimwengu kwenye wakati huo, kusikia hekima ya Sulemani.

¹⁷⁰ Na watu wanaishi upande wa pili wa mtaa na hawatakuja kusikia kitu kilicho kikuu zaidi. Si ajabu Yesu alisema “huyo ataamka katika siku za mwisho na kukihukumu kizazi hiki kwamba kimekosa”!

¹⁷¹ Alikuwa na matatizo njiani. Kumbukeni, wana wa Ishmaeli, hao waendes haji misafara huko nje walikuwa wanyang’anyi jangwani. Jinsi ambavyo ingekuwa rahisi kwa kundi kubwa la hao Waishmaeli kumwangukia maskini malkia huyo na kuwaua hao matoashi nusu dazani, na kuchukua hazina yao yote.

¹⁷² Lakini kuna njia moja ama nyingine, kwamba wakati moyo unapoanza kumwonea Mungu njaa, shida hazionekani kama chochote. Nia yako imeelekezwa, haijalishi mtu yeyote anakuita kitu gani. Wanaweza kukuita chochote wanachotaka kukuita, wanaweza kusema chochote wanachotaka kusema, wanaweza kujaribu kuweka kila jiwe la kikwazo njiani mwako; bali ikiwa unamwonea Mungu kiu, unaenda kupata Hilo mahali fulani. Hayo tu, unaona. Hakuna kitu kinachoenda kukusimamisha. Mume hatakusimamisha. Mke hatakusimamisha. Kanisa halitakusimamisha. Mchungaji hatakusimamisha. Hakuna chochote kinachoweza kumweka mtakatifu mbali na Mungu wake, ikiwa kwa kweli anataka kuona Hilo. La.

Yeye hata hakuwazia hilo.

¹⁷³ Wala na wewe huwazii, kile *huyu* anaenda kusema, na kile mama anaenda kusema, na baba anaenda kusema, ama mume anaenda kusema. Ukija kumpata Yesu Kristo kuwa halisi, na usikie kwamba Yeye yu hai, hakuna kitu kinachoenda kukusimamisha, wakati hiyo njaa, hiyo mbegu ambayo imekusudiwa kimbele kabla ya msingi wa ulimwengu. Wakati Nuru ikiangaza hiyo, inakuja kwenye Uzima upesi hivyo.

¹⁷⁴ Maskini mwanamke huyu alikuwa mbegu ya aina hiyo, hata hivyo akiwa ni mgeni, kafiri.

¹⁷⁵ Sasa, sasa kumbukeni, yeye labda ilibidi asafiri usiku, kulikuwa joto sana kwenye hilo Jangwa la Sahara. Na—na yeye alikuwa amesafiri usiku. Labda akisoma magombo. “Sasa, tutaona kile ambacho nabii alisema hapa kuhusu kile Mungu alichokuwa. ‘Nitafunua siri za moyo. Na akiwepo mmoja miongoni mweni, aliye wa kiroho au nabii, Mimi Bwana nitajitambulisha Mwenyewe kwake, nizungumze na yeye katika maono. Na kile asemacho kinakuja kutimia, msikieni.’ Nitaona nikifika huko. Hicho ndicho Mungu huyo alicho. Nitaona.”

¹⁷⁶ Tazama sasa, baada ya muda mfupi hatimaye aliwasili kwenye uamsho uliokuwa unaendelea. Ulikuwa ni uamsho. Kwa hiyo, aliwasili. Sasa hakuja ili tu kusema, “Nitaingia ndani na niketi chini dakika chache. Na nikimsikia akisema neno moja ambalo kanuni yangu ya imani haikubaliani nalo, ninasimama na kuondoka!” La, yeye anaenda kuwa kwenye Hukumu, kuhukumu wa aina hiyo, unaona. Alikuwa kukaa mpaka alikuwa ameshawishika kabisa.

¹⁷⁷ Kama tungeweza tu kufanya hilo, kuwa tu na kicho na kukaa kimya, na kusema sasa, “Hiki ni kitu ambacho huenda kikaonekana kama kinaweza kuwa sahihi. Sijui. Siendi kukosoa. Ninaenda tu kuketi kimya, na ninaenda kutazama. Ndipo basi ninaenda kukilinganisha na Maandiko na kuona kama ni sahihi.” Unajiwia hilo mwenyewe.

¹⁷⁸ Sasa, alikuja kutoka pande za mwisho za ulimwengu. Alitoka akaingia labda kwenye mabaraza ya hekalu, na akatundika mahema yake na chochote zaidi. Na labda... Sasa ninaenda kuigiza hili kwa ajili ya jamaa wadogo, na kadhalika.

¹⁷⁹ Labda asubuhi hiyo, wakati kanisa lilipofunguliwa, parapanda ikalia, makuhani wakapiga parapanda na muziki ukacheza, na kadhalika. Na nanii wote—watoto wakaanza kukusanyika ndani, na labda alijipatia kiti huko nyuma upande wa nyuma. Kwa kawaida hivyo ndivyo hufanyika. Na akaenda nyuma upande wa nyuma. Vema, alitazama wakati mchungaji Sulemani alipojitokeza. Ndipo yeye... Walimtambulisha na yeye alizungumza na watu na akasoma Maandiko, nao wakaomba. Ndipo basi kisa cha kwanza kikaja.

Sasa yeye atasema, “Nitaona tu ni utambuzi kiasi gani huu ulio.”

¹⁸⁰ Na wakati alipoona utambuzi huo, nadhani mkutano uliofuata alisogea viti vichache mbele. Labda yeye. . . Na hilo, hili, ikiwa sisi. . . Ikisikika ya kukufuru, mnisamehe. Labda kadi yake ya maombi haikuitwa jioni hiyo moja tu, unaona, ilimbidi kungojea kidogo. Ninajaribu kuleta kitu fulani kwa watu, mnaelewa, unaona. Na labda haikuwa hiyo, lakini, hata hivyo, hatimaye alitazama kisa baada ya kisa, naye akashawishika.

¹⁸¹ Lakini ngoja mpaka ifanyike kwake. Hiyo ndiyo anayotamani. Na Biblia ilisema kwamba, “Wakati alipoletwa mbele za Sulemani, kwamba hakukuwa na chochote, swali lolote niani mwake, ila kile ambacho Sulemani alifunua.” Mungu alimfunulia, alimfunulia Sulemani, mambo yote aliyokuwa anahitaji katika maisha yake. Na wakati alipofanya hili, ilimfanyikia wakati huo. Ndipo akasimama, na akasema, “Yote ambayo nimesikia yalikuwa sahihi, na zaidi ya haya.” Akasema, “Na heri ni wale watu ambao huketi hapa kila siku na kuona karama hiyo kuu ikifanya kazi, ishara hiyo kuu. Heri ni wale watu ambao wako pamoja na wewe hapa na kuona mambo haya kila siku.” Alimkubali Mungu. Alikuwa ameona kitu fulani halisi. Moyo wake ulifanywa kuvuma. Alipata kitu ambacho kilikuwa halisi, kitu ambacho hakikuwa kanuni ya imani iliyokufa, kitu fulani ambacho hakikuwa sanamu. Kilikuwa ni Mungu aishiye.

¹⁸² Sasa, si ajabu Yesu alisema kwamba, “Malkia wa Kusini atasimama katika Hukumu, pamoja na kizazi hiki, na kukihukumu kwamba kimekosa; kwa kuwa yeye alitoka pande za mwisho wa dunia, kusikia hekima ya Sulemani, na, tazama, aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa.” Na hata katika siku za Bwana Yesu, Imanueli, Mungu aliyefanyika mwili, “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake,” Yeye alikuwa ni Neno lililo hai. Na katika siku hiyo, hata kuwaambia wale waliopinga huduma Yake ya aina hiyo, kwamba Yeye angewasamehe. Kasema kwamba, “Wakati Roho Mtakatifu alipokuja. . .”

¹⁸³ Mna elimu ya miaka elfu mbili zaidi kwenye Biblia kuliko waliyokuwa nayo kule, miaka elfu mbili zaidi ambayo Roho Mtakatifu amekuwa akitembea duniani. Sasa, kama akihukumu kizazi hicho, atafanya nini na kizazi hiki? Aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa! Maskini mama huyo aliona kitu halisi.

¹⁸⁴ Nimesema jambo hili dogo hapo kabla, lakini ninaamini linastahili kusemwa sasa hivi kabla sijaitisha mstari wa maombi. Ninapenda kuwinda. Mimi—mimi. . . Ni asili tu ya pili kwangu mimi. Ni—ninakupenda. Wongofu wangu kamwe haukuondoa hilo kwangu, kwa sababu ninapenda kuingia nyikani. Nilikuwa nikiwinda juu Kaskazini hapa, na nilikuwa nikiwinda hapa

katika Adirondack, miaka iliyopita. Na ningetoka pale nje na kuenda juu ya milima, nikitazama jua likichomoza na kutua, na kulia, na nikae huko nje kwa majuma, na kumsikia Mungu akizungumza kupitia maumbile. Hapo ndipo Yeye. . .

¹⁸⁵ Biblia yangu ya kwanza ilikuwa maumbile. Kuona jinsi mbegu ndogo ingeanguka ardhini, na kuganda kwa kilindi *hivyo*, na mbegu kupasuka na kufunguka, sehemu nyororo inatoka, na kila ishara imetoweka ambayo unaweza kuona, lakini majira ya kuchipua yanayofuata inaishi tena. Unaona? Mungu alifanya njia kwa ajili yake. “Yeye alifanya njia kwa ajili ya mbegu kuishi tena,” nikasema, “ipo njia fulani kwa ajili yangu kuishi tena.” Hiyo ni kweli. Kwa hiyo hiyo ilikuwa ndiyo Biblia yangu ya kwanza.

¹⁸⁶ Nilikuwa nimezoea kuwinda na mskini Yankee mmoja hapa juu, aliyekuwa mwindaji hodari, lakini alikuwa katili mno moyoni. Na yeye alikuwa—yeye alikuwa mtu mwema, nadhani. Yeye, jamaa mzuri wa kuwinda naye na haikukubidi kusumbuka kuhusu kumsaka, alijua mahali alipokuwa. Basi tuliwinda, bali yeye alikuwa katili sana moyoni mwake. Ndipo nikamwambia, mara nyingi, nikasema, “Kwa nini wewe ni katili sana?”

¹⁸⁷ Na ja—jamaa huyo, si kumdhihaki, au chochote, bali alikuwa na aina ya macho yaliyoonekana kama mjusii. Na yeye—na yeye angenitazama, aseme, “Loo, endelea, mhubiri! Jirudie, Billy! Wewe hutakuwa mwindaji na mhubiri, pia.” Akasema, “Unajua, wewe ni mwoga sana kama kuku.” Na yeye alizoea kuwaua watoto wa kulungu ili tu kunifanya nisikie vibaya.

¹⁸⁸ Jamaa hao wadogo, ninachukia kuwaua. Kwa hiyo akasema. . .Ni sawa kama sheria inasema umwue mtoto wa kulungu, hiyo ni sawa, bali si kuwaua tu kwa ajili ya kujifurahisha. Ibrahimu alimwua ndama, na Mungu akamla. Na hiyo ni kweli, unaona, kwa hiyo si ukubwa wa mnyama. Lakini si kitu ila kumwua tu, kuwa katili, hayo ni mauaji, kwangu mimi. Ninafikiri jamaa huyo mdogo anapaswa kuishi. Kama una haja na yeye, vema, kama sheria inasema unaweza kumchukua, vema, sawa. Unajua, nilikuwa afisa wa uhifadhi kwa miaka saba, kwa hiyo basi kulikuwa na. . .Hiyo ni wakati nilipotumikia kanisa la Kibaptisti.

¹⁸⁹ Kwa hiyo basi wakati jamaa huyu, alikuwa katili sana kuhusu jambo hilo, mwaka mmoja nilienda huko juu, na yeye alikuwa amejitengenezea fi—filimbi ndogo.

¹⁹⁰ Sasa siwatupii hilo watu wa Kibaptisti, unaona. La, unaona, sikumaanisha hilo hivyo. Nilikuwa. . .Sikuwa nje hudumani. Sasa, nilitaka kufanya kazi. Daima nimefanya kazi mpaka wakati tu iliponibidi kwenda kwenye kazi hii ya uinjilisti, na hata hivyo sijawahi kuchukua sadaka maishani mwangu, unaona. Hiyo ni kweli. Unaona? Bali si—sijawahi kumwomba mtu yeyote hata peni moja. Ni—ninataka maisha yangu

yafikie wakati ambapo inanibidi kusema jambo hivi karibuni sana, kama Samueli alivyosimama, alisema, “Je! nimewahi kuwaambia chochote katika Jina la Bwana ila lile ambalo limekuja kutimia? Je! nimewahi kuchukua fedha kutoka kwenu, riziki yenu?” Unaona, hiyo ni kweli. Wakasema, “La, hujawahi.” Lakini walitaka mfalme wao kwa vyovyote vile, kwa hiyo—kwa hiyo hiyo labda ndiyo njia itakayotokea, kwa hiyo daima hufanya hivyo.

¹⁹¹ Lakini jamaa huyu, nilimpenda, na majira fulani ya mapukutiko nilienda huko juu. Na yeye alikuwa amevumbua filimbi ndogo ambayo angeweza kupuliza, kama tu maskini mtoto wa kulungu, huyo ni kulungu mchanga akimlilia mama yake. Kwa hiyo sasa alisema, “Wewe, ninataka kukuonyesha kitu, Billy.” Na yeye alikuwa na filimbi hii ndogo ambayo angepuliza.

Nikasema, “Wewe, usingefanya hivyo.”

¹⁹² Ndipo akasema, “Loo, wewe hapo. Hutaishinda, sivyo?”

Na mimi nikasema, “La, bwana. Si kuwa namna hiyo.”

¹⁹³ Kwa hiyo tu—tukaenda kuwinda, na msimu ulikuwa umeenda sana. Ilinibidi kupanda juu. . . Na nyinyi nyote, wawindaji hapa ndani, mnajua hao kulungu wadogo wenye mikia myeupe huko. Houdini si bingwa wa kutoroka hata kidogo, kwao, kwa hiyo wakati wametishwa. Na kwa hiyo walikuwa wametupiwa risasi. Na kulikuwa na mikondo midogo ya theluji ilikuwa ardhini, maskini. . . kile tunachokiita maskini mashua nyepesi, huko chini Kusini, yapata inchi nne au tano, nzuri ya kutosha kuandama. Na tulienda yapata nusu siku, na nikawazia kwamba. . .

¹⁹⁴ Tulibeba ma—maskini chupa ya themosi iliyojaa chokoleti moto, ambayo hiyo hukupa nguvu, na sandiwichi. Na kwa kawaida sisi huketi chini. Na wakati tukienda juu kwenye kilele cha milima, ndipo anateremka chini kupitia safu moja, na mimi ningeteremka kwa nyingine; tukirudi, tuingie kwenye kambi wakati fulani usiku huo. Kwa hiyo nilifikiria. . . Ilikuwa yapata saa tano, au kitu fulani, na mimi nikafikiria angeketi tu chini juu ya hifadhi ya theluji pale, mahali padogo, uwazi yapata ukubwa wa chumba hiki mara mbili. Ndipo akaketi pale. Nikafikiria tulikuwa tunaenda kula chakula chetu cha mchana, na nikaanza kutoa chakula changu cha mchana.

¹⁹⁵ Ndipo akatoa filimbi hii ndogo, na alikuwa anaenda kuipuliza maskini filimbi hiyo. Na kulungu ni waoga sana namna hiyo, wataishi chini ya malundo ya misitu na kila kitu, wakati majira ya kuwinda yakiendelea. Inawabidi kufanya hivyo, ili kunusurika. Basi yeye—yeye akapuliza maskini filimbi hii. Na alipofanya hivyo, upande wa pili tu wa upenyo huo, kulungu jike mkubwa mnene akasimama. Sasa, kulungu jike ni mama kulungu, na yeye akasimama. Nami nikamwangelia.

Alikuwa mrembo, na hapo hayo masikio makubwa na macho makubwa mno ya hudhurungi. Na—na yeye alikuwa akimtafuta mtoto huyo.

¹⁹⁶ Ndipo akanitazama, namna *hiyo*. Nikawaza, “Hutafanya hivyo, Bert, hakika hutafanya.” Kwa hiyo akatia risasi kwenye bunduki yake. Na yeye alikuwa bingwa wa shabaha.

¹⁹⁷ Nami nikamwona, akaipuliza tena. Naye mama kulungu akatembea moja kwa moja akiingia katika upenyu huo, mnamo saa tano mchana. Sasa, hilo si la kawaida. Hawatafanya hivyo, la, hasa katika msimu wa kuwinda, wakati huo wa mchana, kwa vyovyote vile. Akatokea hapo nje. Kwa nini? Yeye—yeye alikuwa ni mama. Asili yake ilikuwa ni mama. Alikuwa mama moyoni mwake, na mtoto wake alikuwa katika shida. Na yeye alikuwa akimwita, naye alikuwa akimtafuta mtoto huyo.

¹⁹⁸ Nikawaza, “Hakika wewe si katili kutosha kumwua mama huyo akimtafuta mtoto wake!” Alinitazama, namna *hiyo*, na macho ya mjesi. Ndipo a—akachukua bunduki hiyo na kuisawazisha. Nikawaza, “Loo, jamani, hakika hatafanya hivyo.” Na mama huyo hodari akitembea huko nje, amesimama pale!

¹⁹⁹ Ndipo wakati ki—kia ilipoteremka kwenye bunduki, kufungia risasi katika chemba; wakati kia ilipoteremka, kulungu aliisikia hiyo kia, na akageuka akamwona mwindaji. Alikuwa ameinua *hivi* kumpiga risasi, na, jamani, eneo hilo la shabaha kupitia moyo wake mwaminifu! Nikawaza, “Ile risasi kubwa ya thelathini-sufuri-sita, risasi yenye uzito wa mia moja themanini, italipua moyo wake moja kwa moja kutoka ndani yake.” Nikawaza, “unawezaje kufanya hivyo? Mama anayetafuta . . . Na kumdanganya, kuita kana kwamba ni mtoto wake. Na kumtoa hapo nje na kisha unampiga risasi, na moyo mwaminifu ukidunda namna hiyo, unawezaje kufanya hivyo? Kitu gani, unawezaje kuwa katili hivyo?” Ndipo nikamwona akisawazisha. Naye kulungu, badala ya kutoroka kama vile angefanya kikawaida, yeye alisimama tu kimya. Hakuogopa kufa. Mtoto wake alikuwa katika shida.

²⁰⁰ Sasa, angalia, yeye hakuwa tu anajifanya. Hakuwa tu anajifanya. Ilikuwa ni kifo. Unaona? Lakini asingeweza kuliepuka hilo, yeye alikuwa ni mama. Hiyo ilikuwa ni asili yake, mama; na mtoto wake, alikuwa anamtafuta. Alikuwa analia, na yeye alikuwa akimtafuta mtoto wake.

²⁰¹ Nisingeweza tu kuangalia tendo hili likitukia. Nikageuza kichwa changu. Nikaanza kuomba. Nikasema, “Bwana Yesu, usimruhusu afanye hivyo. Usimruhusu afanye hivyo. Anawezaje kufanya hivyo? Maskini mama huyo amesimama pale, na yeye anaenda kulipua moyo wake kutoka kwake.” Vema, nilingojea, na bunduki haikufyatuka.

²⁰² Ndipo nikageuka kutazama, na mtutu ulikuwa ukienda namna *hii*. Asingeweza kuishikilia tena. Ndipo akageuka, akanitazama, na kutoka kwa yale macho kombo kukaja machozi makubwa mazito yakitiririka chini mashavuni mwake. Alinyakua bunduki na kuitupa chini. Na kunishika kwa mguu wa suruali, kwenye huo mkondo wa theluji; akasema, “Billy, yamenitosha. Yamenitosha. Niongoze kwa huyo Yesu unayenena habari zake.”

²⁰³ Kulikuwa na nini? Aliona kitu halisi. Aliona kitu ambacho hakikuwa cha kuigiza. Loo, laiti tungaliweza tu kuwa Mkristo ambaye yule kulungu alikuwa mama. Unaona?

²⁰⁴ Hata hivyo Yesu alisema, “Je! mama angeweza kumsahau mtoto wake anayenyonya? Naam, angeweza. Bali siwezi kuwasahau. Majina yenu yameandikwa kwenye vitanga vya mkono Wangu.”

Hebu tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda mfupi tu.

²⁰⁵ Ni wangapi walio katika Uwepo wa Kiungu wakati huu, tunapoharakisha, wangesema upesi, “Mungu, ninakuomba Wewe unifanye Mkristo mzuri kama yule kulungu alivyokuwa mama, kwamba nitakuwa bila woga. Nitaninii... Ninapenda, ninataka kukupenda Wewe jinsi yule kulungu alivyopenda, mama alivyompenda mtoto wake”? Inua mkono wako, useme... Mungu akubariki. Mungu akubariki. Kuwa upendo wa namna hiyo.

²⁰⁶ Baba yetu wa Mbinguni, wapo wale wanaoketi hapa, wengi, naam, mamia waliinua mkono wao, kwamba wangependa kuwa na tukio hilo. Sababu yule kulungu angeweza kuonyesha ule umama, ule ushujaa, ni kwa sababu yeye alikuwa mama. Asili yake ilikuwa mama. Ee Mungu, tufanye Wakristo, asili yetu Wakristo, Bwana. Si kitu tu cha kujifanya, kusema, “Mimi ni mfuasi wa *hili* ama *lile*,” bali tufanye Wakristo moyoni. Lipande Neno Lako na upendo ndani ya mioyo yetu, Bwana, kwamba tutaweza kuwa, na kuwakilisha kwa ulimwengu, onyesho la Ukristo na upendo wa kiungu, ambao maskini yule kulungu alionyesha siku ile, ya umama. Tujalie, Baba. Ninaomba kwa ajili ya kila mmoja ambao waliinua mkono wao. Jalia tukio hilo lije juu yao.

²⁰⁷ Labda kuna wengine hapa ambao hawajui zaidi ya kujiunga tu na kanisa. Hawajawahi kuona chochote halisi. Bali aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa, Yesu Mwenyewe, ambaye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Naomba kusanyiko linalosubiri, katika kutazama mstari wa maombi usiku wa leo, liona onyesho la upendo wa Mungu na Kweli ya Mungu, kwamba Neno Lake ni Kweli, kwamba Yeye hajafa. Yu hai milele. Na katika kuona haya, naomba wasalimishe maisha yao kikamilifu Kwako, na wawe watoto Wako; na kuwa na upendo mioyoni mwao, ambao hata ungewapeleka mautini, bila woga wowote.

208 Kama Daudi alivyosema, “Naam, nijapotembea kupitia bonde la vivuli vya mauti, sitaogopa uovu wowote.” Kama yule mama kulungu akitembea kutoka mwituni, moja kwa moja kuingia katika vivuli vya mauti, moja kwa moja kuingia katika uwazi. Naye Daudi alisema, “Nitaenda kupitia bonde la kivuli cha mauti. Sitaogopa uovu wowote, Wewe uko pamoja nami.” Mungu, hilo ndilo sote tunataka kuwa. Tujalie, Bwana. Ninaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

209 Bwana awabariki. Ninasikitika kuwaweka muda mrefu sana. Ninaonekana tu kwamba ni vigumu kwangu kuacha kuzungumza. Lakini tunaenda kuwaomba wagonjwa sasa. Ningetaka kwamba wote kwa namna fulani mngebakia vitini mwenu, kwa dakika chache tu. Niliahidi kuweka mstari wa maombi upite, usiku wa leo. Ninataka kufanya hivyo. Na ninajua tunapaswa kufunga hii mapema kuliko hivi, bali ni—ninajua tuko karibu... Pia—pia msimamizi, kwa hakika ninathamini wema wako, bwana, si kung’oa taa. Naomba Nuru ya Mungu iangaze ndani ya maisha yako kama Hiyo haiko humo sasa, ikupeleke Utukufuni siku moja.

210 Sasa yu wapi Billy? Ni kadi zipi ulizotoa? A, kuanzia moja hadi mia moja. Vema. Wanapata, moja kwa moja tukiwa na haraka... Kwa kawaida sisi—sisi huzichanganya. Na wakati mvulana huyo akitoa kadi za maombi, yeye huzichanganya, moja kwa moja mbele zenu, na kukupa tu kadi ya maombi utakavyo, unaona. Kwa hiyo zote zimechanganywa. Kamwe hatujui mahali tunaenda kuanzia kuita. Wengi hapa wamekuwa katika mikutano hapo kabla. Hiyo ni ili kwamba mvulana huyo asiweze kuuza kadi ya maombi, ambalo tulimshika jamaa mmoja akifanya wakati mmoja. Tusingefanya hivyo. Wala na yeye hajui.

211 Anasema, “Vema, wewe nipe kadi hii, hivi nitaingia mstarini?” Yeye hajui. Kwa kuanzia, zote zimechanganywa, na yeye—yeye hukupa tu kadi. Na basi hajui, na mimi sijui mpaka tunapokuja hapa. Kwa kawaida mimi huhesabu idadi fulani katika safu *hii*, na kugawa na idadi fulani katika safu *hii*, na kupata jibu kwa njia fulani, au kuanzia tu mahali fulani.

212 Bali usiku wa leo tunaenda kuacha hiyo, na kuanzia tu kutoka namba moja, kwa sababu tumechelewa. Na kadi ya maombi... Hebu tusimame sasa mmoja mmoja tu, ninapoita namba yako. Ikiwa huwezi kusimama, mtu fulani atakusaidia na kukuleta hapa juu.

213 Sasa ni wangapi hapa ndani hawana kadi ya maombi, na wewe ni mgonjwa? Omba tu. Mungu na akubariki. Hilo ni jema.

214 Sasa ninataka kadi ya maombi namba moja. Ni nani aliye nayo? Moja kwa moja pale. Waweza kuja hapa, mama, papa hapa? Namba mbili, ni nani aliye na kadi ya maombi A, namba... Je! hiyo ilikuwa A? A, namba mbili. Mbili, ni nani aliye na... Mama huyu hapa, waweza kuja moja kwa moja

hapa, mama? Namba tatu. Njoo moja kwa moja hapa. Nne. Njoo papa hapa, bwana. Tano, ni nani aliye na kadi ya maombi tano, waweza kuinua mkono wako? Huyu mama. Sita. Hii huizuia isiwe kama ulingo wa mchezo, mwajua, ambapo... Hili ni kanisa. Sita, saba. Vema, namba nane. Vema, chukua tu mahali pako, nane. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Nane, tisa, kumi na moja.

²¹⁵ Sikuona kumi na moja sasa, huenda ni mtu fulani kiziwi. Waweza kuangalia kadi ya jirani yako? Kumi na moja, unayo kumi na moja, unayo, mama? Hivi utainua mkono wako? Loo, yeye ni kiziwi, ninaona. Wewe angalia kadi yake hapo wakati akiitwa, unaona. Vema, kumi na moja. Unayo, kumi na moja. Kumi na mbili. Kadi ya maombi kumi na mbili, mama huyu hapa. Kumi na tatu, kadi ya maombi namba kumi na tatu. Ni kumi na tatu, kadi ya maombi kumi na tatu, kumi na tatu? [Ndugu mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Vema, mwangalie mama huyo hapo, unaona. Mama aliye na kofia ya samawati, je! yako ni kumi na ta-... kumi na mbili. Na *wewe* una kumi na tatu, unayo, kumi na tatu? Samahani. Kumi na nne. Vema. Kumi na tano. Ninaamini hao watakuwa karibu kiasi tunachoweza kuchukua moja kwa moja kwenye wakati huu, ninaona tu tunakuwa na msongamano kwenye mstari.

²¹⁶ Sasa wengine wenu, ambao hamna kadi ya maombi. Je! kuna yeyote ambaye yupo hapa kwa mara yao ya kwanza? Hebu tuone mkono wako. Vema, tuna furaha kuwa nanyi usiku wa leo. Je! mmewahi kuwa katika mikutano hapo kabla? Inueni mikono yenu kama mmekuwa katika mkutano. Vema.

²¹⁷ Sasa, mtu yeyote anajua kwamba sisi hatudai kuwa waponyaji. Sisi—sisi hatuwezi kuponya watu. Yesu tayari amefanya hilo. Ila tunadai kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Na ikiwa tunaweza tu kujua na kumtambua Yeye miongoni mwetu, kwamba Yesu yupo hapa! Kama Yeye alisimama hapa, na ungeweza kumwona Yeye kwa macho yako, je! hiyo ingekupatia imani? Hakika. Lakini, unaona, Yeye hatafanya hivyo. Wakati Yeye akija, wakati umekwisha basi; Yeye anakuja kutuchukua wakati huo. Lakini Utu wa Roho Mtakatifu...

²¹⁸ Sasa mtu fulani huenda akaja hapa juu akiwa na makovu ya misumari mikononi mwao, na miiba kote usoni mwao. Huyu angekuwa tu ni mwigaji. Huyu angekuwa ni mwigaji. Yeyote angeweza kufanya hilo. Lakini hata katika hilo, kama halikuzalisha Maisha ya Kristo, bado lisingalikuwa ni Kristo. Unaona? La, lazima yawe ni Maisha ya Kristo sasa.

²¹⁹ Na Biblia ilisema, kwamba, “Yeye ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Sasa nyinyi watu huko nje bila ya kadi za maombi, sasa hebu tuchukue tu kitu fulani, na kusema sasa huku tunapoomba, wewe sema tu, “Loo, Kuhani

Mkuu mashuhuri, Yesu Kristo, Bwana wangu na Mwokozi!" Kama kuna dhambi yoyote maishani mwako, iungame, uiondoe.

220 Na nyinyi katika mstari wa maombi, fanyeni jambo lilo hilo, kwa sababu na ihakikishwe vyema itatajwa moja kwa moja hapa. Unaona? Kama una kosa lolote, ambalo hutaki litajwe hapa jukwaani, toka kwenye mstari. Maana, ni wangapi wanajua hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naam, bwana, itatajwa moja kwa moja hapa. Kwa hiyo iweke chini ya Damu, unaona, kwa hiyo, na—na useme tu, "Nisamehe dha—dhambi zangu na unisaidie kukuamini Wewe. Na mimi ni mgonjwa, Bwana, na ninataka kuwa mzima kwa ajili ya utukufu Wako." Unaona, Mungu haponyi tu kuwa anaponya. Unaona? La. Yeye hufanya hivyo kwa ajili ya Utukufu wa Mungu. Na sisi lazima tuungame makosa yetu na kutokuamini kwetu.

221 Basi mwangalie yule baba ambaye alimleta mtoto mwenye kifafa, ambaye wanafunzi hawakuweza kumtibu. Yesu alisema, "Ninaweza, kama unaamini."

222 Akasema, "Bwana, ninaamini! Saidia kutokuamini kwangu." Unaona? A—a—alilia maana alikuwa na hitaji.

223 Sasa wewe hapo, wewe mwombe Mungu na useme, "Mungu, Ndugu Branham hanijui. Hanijui. Bali ninajua Wewe unanijua, kwa hiyo jalia niguse vazi Lako. Nijalie niguse vazi Lako, maana Wewe ni Kuhani Mkuu. Na ndipo Wewe unene kupitia Ndugu Branham na useme kama Wewe ulivyomfanyia yule mwanamke ambaye aligusa vazi Lako duniani. Kwa sababu, kama Wewe ndiwe Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, 'yeye yule jana, leo, na hata milele,' Yeye itabidi atende kwa njia ile ile.

224 Ni wangapi unafikiri waliamini, siku ile wakati yule mwanamke alipomgusa Yeye na kuenda na kuketi chini? Unafikiri ilishawishi watu kule? Unaona, la—labda ilishawishi. Vema, ingeshawishi. Mbona, sisi Mataifa wa siku hii, sisi tuna shukrani hivyo kwa Yesu. Tunapaswa kuwa na shukrani zaidi. Unaona?

225 Basi maskini mwanamke huyu alimgusa Yeye, akaenda na kuketi chini. Yesu akasema, "Hebu kidogo. Ni nani aliyenigusa Mimi? Ni nani aliyenigusa Mimi?"

226 Mbona, Petro alimkemea, kasema, "Bwana," kwa maneno mengine, "halitakuwa jambo la akili timamu kwako Wewe kusema hilo. Mbona, Wewe unawaziwa vyema miongoni mwa watu, kama Nabii. Kwa nini, Wewe ungewezaje kusema 'ni nani aliyenigusa Mimi,' na kila mtu anakugusa Wewe?"

227 Akasema, "Naam, lakini, vinginevyo, huu ulikuwa ni mguso wa aina tofauti. Unaona? Unaona, nguvu zimenitoka Mimi, uweza."

228 Ndipo Yeye akaangalia kote mpaka Yeye akampata mwanamke huyo, akamwambia alikuwa anatokwa na damu. Ndipo mwanamke huyo akahisi mwilini mwake mwenyewe kwamba kulikuwa kumekoma, kwani Yeye alisema, “Imani yako imekuokoa.” Unaona?

229 Sasa Yeye ni Kuhani Mkuu yule yule. Na sasa laiti ungaliweza tu kumgusa Yeye!

230 Sasa, kunigusa mimi kusingesaidia hata kidogo. Mimi ni kama mume wako tu, kaka yako, baba yako, unaona. Kumgusa mmoja wa wachungaji, kungefanya jambo lile lile tu. Unaona? Lakini mguse Yeye, Yeye Ndiye. Sikujui. Sijui chochote kukuhusu. Nisingeweza kukuponya. Kama ningeweza, hakika ningefanya hivyo; lakini siwezi. Siwezi kufanya kile Yeye amefanya tayari.

231 Sasa kama Yeye alikuwa amesimama hapa, Yeye angejifanya tu Mwenyewe ajulikane kwamba Yeye yuko miongoni mweni. Wazia tu hilo. Sasa sote tunajua tunaelekea kwenye kitu fulani moja kwa moja. Tunaweza kuhisi hilo.

232 Sasa, kuna kweli na uwongo. Zipo njia nyingi sana mbalimbali zinazoelekeza, kusema, “Vema, *hii* ndiyo njia, *ile*.” Hapana budi kuwepo na njia sahihi mahali fulani.

233 Na kuwazia kwamba Mungu mwenyewe, ambaye anaenda kuwahukumu kwenye Hukumu, kushuka moja kwa moja hapa miongoni mweni na kusimama pamoja nanyi papa hapa! “Popote wawili ama watatu wamekutanika katika Jina Langu, hapo nipo. Unaona, kazi ambazo nilifanya wakati mmoja,” Yeye ataifanya tena. Aliahidi fanya hivyo. “Nyinyi ni mashahidi Wangu; Yerusalemu, Yudea, Jiji la New York, unaona, ulimwenguni kote.”

234 Basi wewe keti tu kimya kabisa, na uombe. Amini kwa moyo wako wote. Usitie shaka. Amini tu kwa yote yaliyo ndani yako, amini (nafsi, mwili, na roho) na Mungu atakujalia hiyo.

Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu.

235 Muumba Mkuu wa mbingu na nchi, yote ambayo nimesimama hapa usiku wa leo na kusema, yatakuwa bure isipokuwa Wewe uje na kuthibitisha kwamba ni kweli. Tumesikia mengi sana, na watu wamesikia mengi sana. Sasa neno moja kutoka Kwako, Baba, litafanya yote kuwa sahihi. Na sisi tunatazamia hilo.

236 Sasa, tunajua kwamba Wewe hunena tu kupitia midomo ya mwanadamu. Uliwafanya wanadamu mawakala Wako. Siku moja Wewe ulikuwa umesimama, Wewe ulisema, ulitazama mavuno na kusema, “Yameiva,” kasema, “ombeni Bwana wa mavuno kwamba Yeye atawatuma wafanyakazi katika mavuno Yake,” na Wewe ulikuwa ndiye Bwana wa mavuno. Lakini Wewe

uliunganisha sana mpango Wako, Wewe na wanadamu pamoja, hufanyi chochote nje ya hiyo.

²³⁷ Sasa ninaomba, Mungu. Na kama tu Wewe utanitia upako, na usiwatie upako wasikilizaji hawa, kuamini, hautafaa kitu. Inabidi tuwe pamoja kama kitu kimoja, kama ndugu na dada. Ninaomba, Mungu, kwamba Wewe utatutia upako pamoja, ili tuweze kuona tena, tena upande huu wa Umilele, Bwana Yesu mtukufu, aliye mkuu kuliko Sulemani kuwa hapa. Tunaomba hayo katika Jina Lake. Amina.

²³⁸ Sasa ninataka tu hili kuwa na kicho mwezavyo kuwa sasa. [Mpiga piano anaanza kupiga *Amini Tu*—Mh.]

²³⁹ Siku moja, kama nikifa, wanaponitia kaburini, watakuwa wanapiga huo, mwajua. Ukisikia kwamba nimeenda, usiamini kwamba nimekufa. Sijafa. Lakini usimame tu mahali fulani, ukisikia kwenye redio au mahali fulani, kuyasoma kwenye gazeti, imba tu wimbo huo (si mtaimba?) na ukumbuke tu kwamba huo ndio, tu “amini tu.”

²⁴⁰ Sasa, katika wasikilizaji, hakuna mtu mmoja katika mstari huo ambaye ninamjua. Ikiwa kila mmoja wenu katika mstari huo ni wageni kwangu, na unajua kwamba sijui chochote kukuhusu, sijui chochote kilicho shida yako. Inueni tu mikono yenu, useme hivyo. Sasa wewe labda ni mgonjwa; pengine si wagonjwa. Sijui. Huenda ni shida za kifedha, shida za nyumbani. Si—sijui.

²⁴¹ Lakini sasa ikiwa maskini mama huyu hapa atakuja tu karibu, unaona. Asante, hiyo ni sawa. Sasa huyu hapa mwanamke mdogo sana wa umri kuliko mimi. Tumezaliwa labda tumeachana kwa miaka, na maili nyingi mbalimbali. Mara yetu ya kwanza kukutana. Sasa yeye yupo hapa kwa kusudi fulani. Si—sijui. Yeye, labda ugonjwa. Si—sijui kilicho shida yake. Chochote kilicho shida yake, Mungu anajua. Na Yeye akifunua hicho, basi yeye atajua kama ni kweli au sivyo.

²⁴² Sasa ikiwa maskini mama huyu angesema, “Ndugu Branham, mimi ni mgonjwa sana. Mimi—mimi... tumbo langu linanisumbua. Ni—nina vipindi vya kifafa, ama—ama kitu kingine.” Yeye anaonekana kama mtu mwenye afya, lakini huwezi kila mara kuenda na hiyo.

²⁴³ Na kama angesema hivyo, ningesema, “Vema, Biblia ilisema, ‘Weka mikono juu ya wagonjwa.’” Hiyo ingekuwa ndiyo njia Ndugu Roberts angemwomba, Ndugu Allen, ama wengi wa watu hao. Hiyo ni huduma yao. Ndipo wangeweka mikono juu yao, waseme, “Shetani, mwachilie, katika Jina la Yesu. Ninakukemea, Shetani,” ama kitu kama hicho. Waseme, “Endelea sasa, umeponywa.” Mwanamke huyo anapaswa kuamini hilo. Unaona, hiyo ingekuwa sawa.

²⁴⁴ Vema, sasa, vipi kama ana dhambi fulani iliyofichika hapo mahali fulani? Ungeweza kumimina mafuta galoni moja juu yake, umpake mafuta mara nyingi uwezavyo, uruke juu chini,

na kupiga mayowe; huyo ibilisi atakaa papo hapo. Dhambi isiyongamwa. Hutaweza kumsogeza. La, bwana.

²⁴⁵ Lakini sasa ikiwa Roho Mtakatifu anaweza kushuka chini na kumwambia jambo fulani ambalo limekuwapo, anajua kama hiyo ni kweli au la, na halafu amwambie kile kitakachokuwapo. Ikiwa kile “kimekuwapo” ni kweli, kile “kitakachokuwapo” kitakuwa sahihi. Hiyo si ni kweli? Sasa hiyo ndiyo fadhili ya Bwana wetu mpendwa, akijaribu kuleta Bibi-arusi Wake pamoja katika siku hizi za mwisho, unaona, kile Yeye alichohidi kufanya. Ni wangapi wangemwamini Yeye kwa moyo wako wote, kama Yeye angefanya jambo kama hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mungu awabariki kwa uaminifu wenu. Sasa hii ni ninii—ninii. . .

²⁴⁶ Kama unataka kusoma. . . Ninakuomba, kama ulinishika nje ya Maandiko, niambie hivyo. Unaona? Niandikie barua au umwambie mmoja wa wachungaji hawa, na uniambie mahali nimekosea. Si—sitaki kuwa makosani. Ninataka kuwa sahihi, na haina budi kuwa ni hili Neno.

²⁴⁷ Sasa hebu tuchukue kidogo tu namna hii, hebu tuchukue Yohana Mtakatifu 4 hasa tena. Huyu hapa mwaname na mwanamke wakikutana kwa mara yao ya kwanza, kama Bwana wetu na yule mwanamke wa Samaria. Walikutana kwa mara yao ya kwanza, ndipo Yesu akazungumza na yeye kwa muda mfupi mpaka Yeye akagundua mahali shida yake ilipokuwa. Shida yake ilikuwa ni utovu wa maadili. Ndipo Yeye akamwambia mwanamke huyo kile kilichokuwa shida yake, na upesi akatambua hilo, kwamba hapana shaka Yeye alikuwa ni nabii. Mwanamke akasema, “Bwana, naona kuwa Wewe ni Nabii.” Kasema, “Tunajua Masihi yuaa. Wakati Yeye atakapokuja, hilo ndilo Yeye analoenda kufanya.”

Yesu akasema, “Mimi Ndiye.” Unaona?

²⁴⁸ Sasa, kama hiyo ndiyo njia ambayo Yeye alijitambulisha Mwenyewe kwa watu jana; Yeye, ikiwa Yeye ni yule yule leo, ingembidi Yeye kujitambulisha Mwenyewe kwa njia iyo hiyo. Sasa, kama Roho Mtakatifu angesema hivyo kwa mwanamke huyo, basi yeye angejua inabidi hiyo itoke kwa njia fulani ya kiroho. Haiwezi kutoka kwa maumbile. Lazima iwe njia fulani ya kiroho. Sasa huenda yeye akasema kama wale Mafarisayo, “Ni Beelzebuli,” basi hiyo ni shauri yake. Anasema, “Ni Kristo,” basi hiyo ni juu yake na Kristo tena, unaona, chochote kile kilicho.

²⁴⁹ Sasa iweni na kicho kabisa. Ninangojea kidogo, kwa ajili ya huo Upako. Huo ndio unaonifanya kusitasita, unaona. Kwa sababu, Huo huenda hata usije hata kidogo. Ikiwa Huo hautakuja, basi tutainamisha vichwa vyetu na kuruhusu wasikilizaji kufumukana, na kurudi kesho usiku na kumwomba Yeye ikiwa Yeye ataninii. . . Yeye hajawahi kunipungukia bado.

Sasa, mbele za mamia ya maelfu, kwa wakati mmoja, Yeye hajawahi kushindwa sasa. Na hatashindwa wakati huu. Ninajua hatashindwa. Ninajua hatashindwa. Unaona, ninajua tu Yeye hatashindwa.

²⁵⁰ Kwa hiyo, unaona, ninalo niani mwangu kwamba umepita wakati wa kufunga. Huwezi kuwa na . . . huwezi kufadhaika, na Roho Mtakatifu afanye kazi kupitia wewe; inakubidi kutulia. Sasa ikiwa kuna malipo yoyote ya ziada usiku huu, nitayalipa, unaona. Jambo ndilo hilo. Shetani, huwezi kutudanganya namna hiyo.

²⁵¹ Ninachukua mamlaka na utawala juu ya kila roho hapa ndani, katika Jina la Yesu Kristo. Sasa ninii tu . . .

Nitazungumza na maskini mama huyu. Sasa ikiwa Roho Mtakatifu, dada, ninii tu . . .

²⁵² Yesu alizungumza na mama huyu kwa muda mfupi tu ili kushika roho yake, unaona, kuona kilichokuwa shida. Ninaamini hilo ndilo Yeye alifanya. Baba alimtuma Yeye huko juu, na alikuwa na haja kupitia Samaria. Lakini Yeye alipofika huko juu, hayo ndiyo yote Yeye aliyojua, Yeye alikuwa huko juu. Hapa anakuja mwanamke huyo, Yeye alijua huo hapana shaka ndio wakati.

²⁵³ Sasa Baba alinituma hapa juu. Mimi hapa, katika New York; na wewe hapa, mtu wa kwanza jukwaani usiku wa leo. Sijui, lakini Yeye atanifunulia. Kama Yeye atanifunulia, je! itakufanya kumwamini Yeye kwa moyo wako wote? Utakubali? Utajua kama ni kweli au si kweli, unaona. Bila kukujua, na kuwa ni mgeni kwako; bali shida yako, kile wewe . . . Una shida nyingi. Lakini shida yako kubwa ambayo unataka maombi kwa ajili yake, iko katika koo lake. Una tatizo la koo. Je! hiyo ni kweli? Inua mkono wako. Je! unaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hebu kidogo tu. Sasa, hiyo ingekuwa sawa.

²⁵⁴ Unasema, "Huenda umebahatisha hiyo, Ndugu Branham." La, sikubahatisha. Daima mimi hushika hiyo kutoka kwa wasikilizaji, "Alibahatisha hiyo."

²⁵⁵ Sasa kidogo tu, hebu tuzungumze na yeye peke yake. Unajua kwamba kuna jambo fulani linaloendelea, unaona.

²⁵⁶ Sasa kwenye wasikilizaji. Ni wangapi waliona ile picha ya Malaika wa Bwana, ile Nuru? Imening'inia huko Washington, DC. Unaona, Hiyo imening'inia moja kwa moja karibu naye sasa. Unaona? Hivi hamwezi kuona Hiyo? Inaonekana kama . . . Bila shaka, Upako upo hapa sasa. Ninaweza kuona Hiyo, unaona. Iko moja kwa moja juu yake.

²⁵⁷ Naam, Hii hapa. Ana ninii, naam, shida yake iko kwenye koo lake. Amekuwa na wasiwasi. Tena, vema, ana ki—kivimbe katika koo lake. Hiyo ni kweli kabisa. Si hicho tu, bali una tatizo la kikoromeo ambalo linakusumbua. Je! hiyo ni kweli?

Unaona? Vema. Je! sasa unaamini kwamba huyo ni Yesu Kristo amesimama hapa ambaye anakujua na yote kukihusu? Je! unamkubali Yeye kama mponyaji wako? [Dada huyo anasema, “Ninamkubali.”—Mh.] Nenda na uwe mzima, katika Jina la Bwana.

Mstari, unaona, angalia tu. Yeye anajua mambo yote.

²⁵⁸ U hali gani, msichana? Sasa wewe umeshtuka tu kidogo, unaona, kwa sababu punde tu ilipotokea, mama huyo aliposimama, Nuru hiyo ilikuja moja kwa moja juu yake. Unaona? Na yeye anajua. Sasa tazama. Simjui mwanamke huyo. Si—sijui chochote kumhusu. Lakini yeye amesimama hapo, kijana mwanamke tu. Na sasa ikiwa Roho Mtakatifu anaweza kunifunulia kile kilicho shauku yako kutoka kwa Mungu! Wewe ni Mkristo, unaona. Na kwa hiyo ikiwa—ikiwa hukuwa, sasa, Yeye angeniambia hivyo, unaona. Lakini wewe ni Mkristo, ninamaanisha Mkristo halisi. Na kama Yeye angeninii, kama Yeye angenifunulia kile ambacho ni shauku zako kutoka Kwake, je! ungeniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama mtumishi? Ninapaswa kusema hilo, unaona, wakati utawadia, unaona. Ungeamini? [Dada huyo anasema, “Amina.”—Mh.] Unajua kwamba mimi ni mgeni kwako.

²⁵⁹ Sasa, kwa kweli huko hapa kwa ajili yako mwenyewe. Ninaona mwa—mwanamke, mwanamke mwenye umri mkubwa, kweli, ni mama yako. [Dada huyo anasema, “Ndiyo!”—Mh.] A-ha. Na yeye hayupo hapa. Na yeye ni... Umesumbuka sana kumhusu. Yeye amehangaishwa, pia, na kansa. Na unahangaika kuhusu hali zake. Je! unaamini, ewe msichana, kwamba huyo ni Roho Mtakatifu anayefanya hayo? [“Amina.”] Sasa chukua lesa hiyo kutoka kwenye kifuko chako na uende nyumbani. Ukimwona mama yako, ama umtumie hiyo, na—na uweke au utume lesa hiyo kwake kwa ukumbusho wa maombi haya usiku wa leo. Na usitie shaka moyoni mwako. Bali uamini kwamba Yesu... [Dada huyo anazungumza na Ndugu Branham.] Naam, na giza litamwondokea, na yeye atakuwa... Utakuwa mzima. Nenda sasa, na Bwana akubariki. Mungu akubariki, dada yangu.

²⁶⁰ Je! utaamini kwa moyo wako wote? Sasa, kabisa usitie shaka. Kuwa tu na imani.

²⁶¹ Sasa kidogo tu, mniwie radhi kwa muda mfupi tu. Jambo fulani limetukia. Kulikuwa na mtu mwingine aliyetokea hapa. Ni nani yule mama ambaye ndiyo kwanza aombewe hapa, yuko wapi hapa? Loo, naam, hiyo ilikuwa sahihi. Hebu kidogo tu. La. Sekunde moja tu, Roho Mtakatifu... Yupo mtu mwingine amekuja. Unaona, Hiyo ni Nuru, na imeacha...

²⁶² Naam, ni mama huyu mweusi anayeketi papa hapa. Naam, ulikuwa umeketi pale ukiomba kwa ajili ya uponyaji. Sasa, wewe ni mgeni kwangu. Sikujui. Lakini je! unaamini kwamba

Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Je! unaamini shinikizo hilo la juu la damu linaenda kukuacha, na unaenda kuwa mzima? Hilo ndilo ulilokuwa unaombea. Unaona? Amini. Aligusa kitu gani? Hawezi kunigusa mimi, yuko mbali sana na mimi. Alimgusa Kuhani Mkuu ambaye anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.

²⁶³ Amini tu. Sasa, unaona, haikulazimu kuwa hapa juu. Wewe kuwa hapo. Amini tu, hayo ndiyo yote ninayokuomba kufanya. Amini tu.

²⁶⁴ Huyu hapa mama ameketi moja kwa moja hapa nyuma, akiangalia upande huu, akiomba. Anaomba si kwa ajili yake mwenyewe. Anaomba kwa ajili ya mpendwa wake. Kwa sababu kwamba hii... Mtu fulani ndiyo kwanza atoke hapa, ambaye alikuwa akiomba kwa ajili ya mpendwa wake, msichana akiomba kwa ajili ya mama yake. Lakini msichana huyu anaomba kwa ajili ya baba yake. Naye baba yake, ninaona bahari inayovuma, yeye—yeye—yeye si... Anatoka ng'ambo au kitu fulani, Norway, Mnorwe. Hiyo ni kweli kabisa. Mwamini Bwana Yesu, msichana, naye baba yako atapona.

Sasa aligusa kitu gani? Mwulize kama ananifahamu.

²⁶⁵ Je! hilo ndilo ulilokuwa unaombea? Punga mikono yako kama hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Hatufahamiani. Je! hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli. Vema. Unapata haja yako ikiwa tu utaamini.

²⁶⁶ Aligusa nini, yadi ishirini kutoka kwangu? Alimgusa Kuhani Mkuu, unaona, si mimi. Simfahamu mwanamke huyo. Bali alimgusa Kuhani Mkuu, Bwana Yesu mpendwa Yule ambaye yuko pamoja nasi usiku wa leo.

Wewe ni mgeni. Je! huyu ndiye mgonjwa, huyu ndiye mtu huyo?

²⁶⁷ Unaona, inanibidi tu kufuata Hiyo jinsi Hiyo inavyoniongoza, unaona. Kama yule mwanamke, unaona, Yeye alimtambua. Unaona, a—alimgusa Mungu, kupitia Yeye. Vema, hao watu huko nje, hicho ndicho wanachofanya, wanamgusa Mungu. Unaona, ninii tu... Inanibidi kugeuka jinsi Hiyo inavyofanya.

²⁶⁸ Sasa, hatufahamiani mmoja na mwenzake. Sikujui. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Hatufahamiani. Kwa hiyo watu wataona sisi ni wageni, hatufahamiani mmoja na mwenzake. Sasa ikiwa Bwana Yesu sasa angenifunulia kitu fulani ambacho unajua kwamba sijui chochote kukihusu, basi hicho ingebidi kije kupitia Nguvu za kimbinguni. Unaona, uponyaji wa Kiungu, kama unataka uponyaji... Sijui huo ndio unaohitaji, unaona. Wakati mwingine ni kwa ajili ya mtu mwingine, na tatizo la kinyumbani, fedha, na kadhalika. Lakini Yeye anaweza kukidhi yote. Kama Yeye anajua kile unachohitaji, Yeye anaweza kukifunua kwangu, unaona. Ndipo basi kama Yeye akifanya

hivyo, basi unajua ni Yeye. Unaona, unajua haina budi kuwa ni Yeye.

²⁶⁹ Je! hiyo ingewafanya nyote kuamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema, aminini.

²⁷⁰ Sasa, anaonekana kuwa ni mtu mwema. Unaona? Sasa hebu tuongee tu kidogo.

²⁷¹ Sasa Hiyo imeondoka, Hiyo imeenda kwa wasikilizaji. Mtu fulani... Iweni tu na kicho, unaona. Ni ule mvuto mkubwa wa imani. Inaipeleka tu moja kwa moja... Unaihisi, nguvu! Nilihubiri yapata saa moja na nusu, na ono moja hunifanya dhaifu kuliko ninapohubiri saa kumi. Uweza, *nguvu* ni “uweza.”

²⁷² Unaona, unafanya hilo. Si mimi. Mimi siye. Maono haya si mimi. Ni wewe unayefanya hilo. Ni imani yako katika Mungu, mimi inayoifanya. Si mimi. Mimi siye. Mimi—mimi nimeketi tu hapa kama mwakilishi. Kama *hiki* hapa, hiki ni—hiki ni bubu, kipaza sauti hiki, isipokuwa kuwe na sauti hai inayonena kukipitia; hakiwezi kuzungumza, chenyewe. Wala nami siwezi kunena. Ni Yeye, Yule aliye hai, Kristo, Yule aliye hai, Yeye hunena na Yeye anajua kuwa wewe ni nani na kile ambacho umefanya.

²⁷³ Hebu turudi kuzungumza na mama huyo tena. Ikiwa Bwana Yesu atanifunulia kitu fulani maishani mwako, ambacho wewe... labda kitu ambacho unahitaji kutoka Kwake. Maana, ikiwa mwaminio, u—unamwomba Yeye kitu fulani. Na kama Yeye atanifunulia hicho, je! unaamini kwamba ungekipokea? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Ungekiamini? Sasa, shida yako iko katika tumbo. [“Ndiyo.”] Uchunguzi umeonyesha kwamba tumbo lako limeshuka. [“Ndiyo.”] Hiyo ni kweli. Je! hiyo ni kweli? [“Ndiyo.”] Na hiki hapa kitu kingine katika uchunguzi, wamekuta unacho kivimbe ndani ya tumbo lako. [“Ndiyo.”] Je! hiyo ni kweli? [“Ndiyo.”] Je! unaamini? [“Ndiyo.”] Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia kuwa wewe ni nani? [“Ndiyo.”] Bibi Willard, wewe endelea uende nyumbani sasa na uamini.

²⁷⁴ Wewe, je! unaamini kwa moyo wako wote? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa mwulize mama huyo. Hatujawahi kuonana maishani. Bali, ni Roho Mtakatifu, Yeye yupo hapa. Sasa iweni na kicho kabisa. Mniambie wakati mkiwa na muda wa kutosha sasa, unaona, ambapo...? . . .

²⁷⁵ Sasa, u hali gani, bwana? Sasa hatufahamiani mmoja na mwenzake. Na unatambua kwamba siku moja inabidi tukutane na Mungu. Na kwa kuwa mgeni kwangu, na mimi kwako, ikiwa Bwana Yesu angenifunulia shida zako, je! ungeamini kwamba ni Yeye? Na unajua kwamba mimi, mwanadamu, nisingeweza kujua hilo. Lakini ingemchukua Yeye kufanya hivyo. Je! hiyo ni kweli?

276 Ninachukia kusema hili. Mvulana huyo ametiwa uvuli, unaona, kuna giza juu yake. Tena ni—ni kitu cha hatari sana kilicho kasoro. Una kansa. Hiyo ni kweli. Na eksirei imeonyesha na kufunua kwamba kansa hiyo iko kwenye tumbo, na tena iko kwenye ukuta wa tumbo. Iko juu ya... Je! hiyo ni kweli? Hapo ndipo ninapoiona picha hiyo, eksirei. Iko kwenye ukuta wa tumbo. Sasa hiyo inamaanisha kwamba huna budi kuondoka hivi karibuni; la sivyo, Mungu akusaidie. Je! utakubali hilo, ndugu yangu? Yesu... Kansa si kitu kwa Yesu Kristo, si zaidi ya kuumwa na kichwa. Je! unaamini hilo? Sasa jambo fulani ndiyo kwanza litukie ndani yako. Ulikuwa na hisia nzuri kwelikweli, unaona. Sasa kama utaendelea kuamini namna hiyo! Kivuli hicho kimekuacha. Unaona? Imani yako ilikuokoa. Nenda, ukiamini sasa, naomba Mungu atakufanya mzima.

277 Mungu anaweza kuponya baridi yabisi. Hivi huamini hilo? [Mgonjwa huyo anasema, “Amina.”—Mh.] Vema, anza tu kutembea, ukisema, “Asante, Bwana Yesu.”

278 “Kama unaweza kuamini! Mambo yote yanawezekana kwa hao ambao—ambao wanaamini.” Vema.

279 Kwa namna fulani ilikufanya ujihisi kiajabu wakati niliposema “baridi yabisi.” Hiyo ndiyo uliyo nayo, pia, ni vigumu kwako kusimama, asubuhi, hukukausha. Imekwisha sasa, kama utaamini. Rudi nyuma, nenda uamini hilo. Bwana akubariki. Amini tu hilo.

280 Ugonjwa wa pumu hapo, unaona. Je! unaamini Mungu anaweza kuponya huo? [Mgonjwa huyo anasema, “Amina.”—Mh.] Mpokee Yeye, nenda na Yesu Kristo anakufanya mzima, na uamini kwa moyo wako wote.

281 Unataka kuenda kula chakula chako cha jioni, ukifurahie; shida ya tumbo imeisha, na uende na uwe mzima? Nenda, amini hilo. Kama unaweza kuamini!

282 Mungu anaweza kuponya shida ya mgongo, chochote kingine. Hivi huamini hilo? Je! unaamini kwamba Yeye anaweza kuponya yako? Nenda zako, ukishangilia, ukisema, “Asante, Bwana.”

283 Je! unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, au mtumishi Wake? Unaamini Mungu anaweza kuponya tatizo la moyo? Basi nenda, amini hilo.

284 Una tatizo la kike, kitu kimoja, na baridi yabisi. Je! hiyo ni kweli? Je! unaamini Yeye ndiye mponyaji wa Kiungu? Mkubali Yeye kama Mponyaji wako. Nenda ukishangilia, ukisema, “Asante, Bwana.”

285 Una tatizo la kike ambalo limekusumbua kwa muda mrefu. Pia una tatizo la moyo. Liko karibu tu kukuuu. Una ninii—una kudunda, moyo unaodunda pole pole. Amini kwa moyo wako wote, na halitakusumbua tena. Nenda, na uamini.

²⁸⁶ Ugonjwa wa damu. Je! unaamini kwamba Mungu anaweza kuifanya hiyo damu, arudishe hali hiyo ya upungufu wa damu, na kuiponya? Je! unaamini hilo? Vema, nenda ukiamini, hicho kisukari hakitakusumbua tena. Wewe amini kwa moyo wako wote.

²⁸⁷ Je! unaamini kwamba Yeye amekuponya wewe unayeketi hapo? Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Unaamini ni Mungu, anayekufanya mzima kabisa, kikamilifu? Mungu akubariki. Nenda zako na ushangilie. Amina.

²⁸⁸ Shida hiyo ya mgongo haitakusumbua tena, ingekufanya ujisikie vizuri sana, sivyo? Vema, nenda ukishangilia, useme, “Asante, Bwana Yesu,” na uamini kwa moyo wako wote.

²⁸⁹ Damu, katika damu yako, inadondoka nyepesi; kisukari. Je! unaamini kwamba Mungu anaweza kuponya kisukari? Hebu tuende Kalvari kwa nyongeza ya damu. Yeye atakiondolea mbali kutoka kwako.

²⁹⁰ Una shida ya kifua. Sivyo? Nilikuwa ninaenda kukuita, dakika chache zilizopita. Dakika chache tu zilizopita ulikuwa ukinitazama, ndipo nikageuka na kukutazama, na ulishika jicho langu na kutazama chini; hisia ya ajabu kwelikweli ilikuja juu yako, shida ya kifua ilikuacha. Imekwisha. Ilikuwa ni hali ya mishipa iliyofunga kifua chako. Wewe amini.

²⁹¹ Unawazia nini huko nje, ukiwa na hiyo baridi yabisi, ukiwa umeketi mwishoni mwa kiti, je! unaamini? Simama, Yesu Kristo anakufanya mzima.

²⁹² Nakusai kumwamini Mungu, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele! Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Kama mnaamini kwa moyo wenu wote, wekeaneni mikono yenu mmoja juu ya mwingine. Yeye hawezi kushindwa. Yeye ni Mungu, mpendwa Bwana Yesu, nguvu Zake zilizofufuka, utambulisho Wake. Kila mmoja wekeaneni mikono mmoja juu ya mwenzake.

²⁹³ Baba wa Mbinguni, adui yuko mbioni. Adui ameshindwa. Yesu Kristo anaishi na kutawala. Ee Mungu, turehemu na ujalie uponyaji wa watu hawa.

²⁹⁴ Shetani, umeshindwa vita! Yesu Kristo ame—amepata ushindi katika ukumbi huu usiku wa leo. Umefichuliwa. Wewe ni mdanganyifu tu; na sisi tunaitisha mkono wako, katika upendo wa Kalvari. Toka ndani ya watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo, na uwaache na kuwaachilia huru!



ISHARA YA WAKATI HUU SWA63-1113

(The Sign Of This Time)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, tarehe 13, Novemba, 1963, katika Marc Ballroom kule New York, New York, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org